epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Juni 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581717
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 2

## MFANYAKAZI WA TANAPA, FAMILIA WATEKETEA KWA MOTO

MFANYAKAZI wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania...

UKURASA WA 4

## TLS YATAJA SABABU MKWAMO MCHAKATO KATIBA MPYA

RAIS wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Harold Sungusia, amesema moja ya chanzo kikubwa...




UKURASA WA 5

## UCHUMI KIDIJITI KUKUA KUMALIZA CHANGAMOTO KIMTANDAO

UCHUMI wa kidijiti unatarajiwa kukua zaidi nchini...

UKURASA 21

## RONALDO ASIMAMISHA MECHI EURO MARA NNE

# TUCTA yataka usawa mifuko PSSSF, NSSF kikokotoo

UKURASA 2




Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, akizungumza wakati wa kikao cha dharura cha kamati tendaji ya shirikisho hilo, juu ya maoni yao kuhusiana na bajeti ya serikali kwenye mkupuo wa kikokotoo cha mafao mkoani Morogoro jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Serikali kukutana na wafanyabiashara K'koo leo

UK.4



"Katiba ya Zanzibar imedhihirisha kuwa kila baada ya miaka mitano kutakuwa na uchaguzi na uzuri wa Katiba ya Zanzibar jambo lolote la kubadili lazima uitishe kura ya maoni na gharama zake ni sawa na uchaguzi mkuu...

**Salum Bimani**



"Tangu Mapinduzi ya Zanzibar hakuna Rais wa Zanzibar aliyepindukia ukomo wa miaka iliyowekwa kikatiba...

**Pandu Ameir Kificho**



"Wajumbe wa sekretarieti tumejadili na kutathmini kwa kina juu ya utendaji wa Rais Dk. Mwinyi, tukajiridhisha kuwa hakuna mbadala wake na anastahili aongoze nchi kwa kipindi cha miaka saba...

**Dk. Mohamed Dimwa**

# Wadau wapinga Rais wa Z'bar kuongezewa muda

UKURASA 3





Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Dk. John Stephen Simbachawene, kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# TUCTA yang'ang'ania usawa kikokotoo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limeishauri serikali kuangalia upya na kuweka usawa katika nyongeza ya mkupuo ya kikokotoo kwa watumishi walioguswa na mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma, ili kuwe na usawa wa asilimia 40 na kuondoa tofauti iliyopo.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya (pichani), alisema hayo jana wakati wa kikao cha dharua cha kamati tendaji ya shirikisho hilo kuhusu Bajeti ya Taifa ya mwaka 2024/25 kilichokutana mkoani hapa.

Alisema watumishi wote ni kundi moja la wafanyakazi wanaotoka kwenye utumishi wa umma kupitia mfuko wa PPF ambao uliunda mfuko wa PSSSF.

Nyamhokya alisema TUCTA inaishauri serikali kufanya mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Sekta Binafsi, kutokana na mabadiliko yaliyopendekezwa kutonufaisha wote na kuigusa PSSSF pekee inayopata asilimia 40 huku NSSF ikiwa imepata asilimia 35.

Akiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya serikali bungeni Juni 13, mwaka huu, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema, serikali inakusudia kuboresha hifadhi ya jamii kikokotoo cha malipo ya mkupuo ya pensheni kiongezeke kutoka asilimia 33 ya sasa hadi 40 kwa wafanyakazi waliokuwa wakilipwa asilimia 50 (PSSSF) kabla ya mifuko kuunganishwa.



Aidha, mapendekezo hayo yanasema asilimia 35 iwe kwa watumishi ambao walikuwa wakipokea asilimia 25 (NSSF) kabla ya mifuko kuunganishwa.

Alisema katika kuhakikisha wastaafu wanapata mafao yao kwa wakati, TUCTA inatoa rai kwa Menejimenti za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuendelea kuwekeza kwenye miradi yenye vihatarishi vichache itakayozalisha faida kubwa ili kuwezesha kufikia lengo la kuwapatia mafao bora wanachama tofauti na hali ilivyo sasa kama ilivyobainishwa na mamlaka.

Rais huyo alisema kamati ya utendaji ya TUCTA ina matumaini kuwa serikali itaangalia kwa upana zaidi vikokotoo vyote vya pensheni pamoja na mafao mengine ya hifadhi ya jamii kwa ajili ya kuyaboresha kwa kuzingatia misingi endelevu ya uendeshaji na usimamizi wa mifuko.

Hata hivyo, aliipongeza serikali kwa kutenga Sh. trilioni 11.77 kwa ajili ya gharama za matumizi ya mishahara ambayo yanajumuisha kupandisha madaraja, ajira mpya, stahiki mbalimbali za watumishi na nyongeza ya mkupuo kwa watumishi wa umma.

Alisema TUCTA inaipongeza serikali kwa kutenga fedha kiasi cha Sh. bilioni 48.3 kwa ajili ya malipo ya bima ya afya kwa wote kwa makundi maalumu.

Hoja ya kikokotoo iliibuliwa na gazeti hili mwaka 2018 baada ya serikali kutangaza Sheria namba 2 ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma mwaka 2018 iliyofuta mifuko ya hifadhi ya jamii ya LAPF, PSPF, GEPF, PPF na kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Mfuko huo ulianza Agosti mosi, 2018 na waliokuwa wanachama wa mifuko iliyounganishwa walihamishiwa PSSSF na kuendelea kuchangia na kupata huduma isipokuwa wanachama wote waliokuwa watumishi wa sekta binafsi kutoka mifuko iliyounganishwa NSSF huku watumishi wa umma waliokuwa NSSF walihamishiwa PSSSF kuanzia Februari 2019.

Kanuni hizo za kikokotoo ziliibua mjadala na Desemba 28, 2018, Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli alisitisha matumizi ya kikokotoo kipya hadi 2023, serikali itakapokuja na utaratibu mzuri wa matumizi yake na hivyo kuendelea na kuwa ni vikokotoo viwili wa asilimia 25 kwa NSSF na 50 kwa PSSSF.

Aidha, mwaka 2023 serikali ilitangaza kupandisha kikokotoo cha mkupuo kutoka 25 ya awali hadi 33 kwa mifuko yote, hatua ambayo bado iliendelea kulalamikiwa na watumishi hasa wa umma ambao awali walikuwa wakipokea asilimia 50 kutoka mfuko wa PSPF.

Hoja zilizotolewa wakati wa kufanya mabadiliko ya sheria hizo ilikuwa ni kuuokoa Mfuko wa PSPF wakati huo usife kwa kuwa ulifikia hatua ya kushindwa kulipa wanachama wake waliostaafu.

Kwa mapendekezo ya sasa kutakuwa na vikokotoo viwili ambavyo ni asilimia 35 kwa watumishi wa sekta binafsi wanaohudumiwa na mfuko wa NSSF na asilimia 40 kwa watumishi wa umma.

# Mfanyakazi wa TANAPA na familia yake wateketea moto baada nyumba kuungua

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MFANYAKAZI wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na watoto wake watatu wamefariki dunia, huku mama yake na ndugu zake wakijeruhiwa baada ya nyumba walimokuwa wamelala kuteketea kwa moto.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani humo, Jeradi Nonkwe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo usiku wa Juni 22.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa chanzo cha moto huo ni kompyuta mpakato (laptop) iliyokuwa imechomekwa kwenye soketi ya umeme kushika moto na kuunguza kochi.

Kwa mujibu wa Nonkwe, moto huo ulisababisha vifo vya watoto watatu papo hapo, huku watu wengine saba, akiwamo mtoto mchanga wa siku nne, wakinusurika baada ya kukimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount.

"Baba mzazi wa watoto hao, Zuberi Msemo, yeye alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru," alisema.

Aliwataja waliopoteza maisha ni watoto watatu, Mariam Zuberi (9), Salma Zuberi (7) na Bisma Zuberi (3) na baba yao mzazi, Zuberi Msemo, ambaye ni mfanyakazi wa TANAPA.

Majeruhi wanaopatiwa matibabu Hospitali ya Mount Meru, ni mama wa watoto hao Jasmine Khatibu (33), Mariam Mussa (60) ambaye ni mama mzazi wa Zuberi na Mwanaid Aldina (50).

Wamo pia, Mussa Msemo (34) AbdulKarim Ramadhan (9) na mfanyakazi wa ndani aliyefahamika kwa jina moja la Ester (20).

Mmoja wa majirani, Ernest Swalehe, alisema akiwa anapita katika eneo hilo asubuhi, akitokea mjini alikompeleka ndugu yake kusafiri, aliona nyumba hiyo iliyoko pembezoni mwa barabara ikifuka moshi, ndio akaanza kuita watu ndani kabla ya kuanza kuamsha majirani wengine.

"Nilipoona kimya na najua hii nyumba huwa ina watu wengi nilipaki pikipiki na kuanza kugonga mageti ya jirani ambao nao waliitika kwa wingi na kuanza kuvunja geti na kuingia ndani, kung'oa madirisha na ndipo tulipofanikiwa kuwatoa watu hao," alisema Swalehe.

HABARI KITAIFA

# Wadau wapinga mapendekezo Rais Z'bar kuongezewa muda

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, amesema Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati Maalum ya NEC CCM Taifa Zanzibar, wamepitisha pendekezo la kuishauri Kamati Maalum ya NEC kuridhia kuongeza muda wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kuongoza nchi katika muhula wake wa kwanza kwa kipindi cha miaka saba badala ya mitano iliyopo kikatiba.

Wadau wa siasa visiwani humo wamepinga pendekezo hilo na kutaka Katiba kuheshimiwa.

Akifungua Mkutano wa Baraza Kuu la UVCCM Wilaya Dimani kichama Zanzibar, uliofanyika katika Ofisi za wilaya hiyo Kiembesamaki, Dk. Dimwa alisema wajumbe hao baada ya kujadili kwa kina wameona kiongozi huyo aongezewe muda.

Dk. Dimwa alisema uamuzi huo wa kumwongezea muda wa kuongoza nchi unatokana na kuridhishwa na kasi yake ya kiutendaji katika kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa zaidi ya asilimia 100 ndani ya kipindi cha miaka mitatu na miezi kadhaa toka aingie madarakani.

Katika maelezo yake, Dk. Dimwa alisema kuwa CCM Zanzibar imeona serikali kuingia katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ni hasara na matumizi mabaya ya fedha za walipakodi kwa kuwa wananchi wanahitaji maendeleo endelevu na Rais Dk. Mwinyi anafaa kuongezewa muda, ili Zanzibar iwe nchi ya visiwa iliyoendelea kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Wajumbe wa sekretarieti tumejadili na kutathmini kwa kina juu ya utendaji wa Rais Dk. Mwinyi, tukajiridhisha kuwa hakuna mbadala wake na anastahiki aongoze nchi kwa kipindi cha miaka saba, ili apate muda mzuri wa kufanya mapinduzi ya kimaendeleo katika nyanja za kiuchumi na kijamii," alibainisha.

Kwa mujibu wa Katibu huyo, maamuzi yao yatafuata taratibu za kikatiba na kikanuni kwa kuyawasilisha katika vikao vya ngazi za juu ili vitoe baraka zake na hoja hiyo ikapitishwe katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Alisema kuwa wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla visiwa vya Zanzibar wanampenda, kumthamini na kuridhishwa na utendaji wa Rais wa Zanzibar Dk. Mwinyi kutokana na uongozi bora katika kutatua kero za wananchi kupitia uimarishaji wa sekta mbalimbali za umma na binafsi.

Alisema kila mwananchi mwenye uzalendo na utimamu wa akili anajua maendeleo yaliyotekelezwa visiwani Zanzibar katika sekta ya afya, elimu, usafiri wa anga na majini, uwekezaji, barabara za kisasa, uwezeshaji wananchi kiuchumi, utalii, michezo na miundombinu bora ya biashara na ujasiriamali.

Kupitia kikao hicho Dk. Dimwa, alifafanua juu ya hoja ya Chama cha ACT-Wazalendo kudai kuwa nchi ina deni kubwa na kusema kuwa suala la mikopo kwa ajili ya uimarishaji maendeleo ya nchi sio dhambi au uvunjaji wa sheria za nchi kwani hakuna nchi yoyote duniani inayojiendesha kiuchumi kwa fedha zake za ndani bila kukopa Benki ya Dunia au nchi zilizoendelea kiuchumi.

**WANASIASA WAPINGA**

Aliyekuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Pandu Ameir Kificho, akizungumza na mwandishi wa habari hizi, alisema suala la kuongeza muda wa urais badala ya miaka mitano iliyowekwa kikatiba kuwa miaka saba ni vigumu kwa sababu nchi nyingi za Jumuiya ya Madola (Common Wealth) zina utaratibu wa miaka mitano wa kipindi cha kwanza cha uongozi. "Mimi wakati fulani nilikuwa na mapendekezo ya aina hiyo ili kusiwe na mizozo ya watu kutaka utaratibu wa kikomo cha miaka 10 iondoke ambao ni utaratibu wa Common Wealth na tangu Mapinduzi ya Zanzibar hakuna Rais wa Zanzibar alipindukia ukomo wa miaka iliyowekwa kikatiba," alisema Kificho ambaye ni mwanasiasa mkongwe visiwani Zanzibar.

Kiongozi huyo ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Bunge la Katiba, alisema utaratibu wa miaka mitano kwa kipindi cha kwanza na isiyozidi miaka 10 kwa vipindi viwili ndivyo marais wengi wa Common Wealth walivyokaa madarakani na baadhi ya viongozi wa nchi hizo hata hawakuendelea na kipindi cha awamu ya pili ya miaka 10.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF, Hamad Masoud Hamad, alisema kuwa ni vyema Katiba ya nchi ikaheshimiwe kwa sababu ndio msingi wa uongozi wa nchi.

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Umma wa Chama cha ACT-Wazalendo, Salum Bimani, alisema, kauli hiyo ya kutaka Rais kuongezewa muda inadhihirisha Chama Cha Mapinduzi kinaogopa uchaguzi mkuu.

Alisema Katiba ya Zanzibar imedhihirisha kuwa kila baada ya miaka mitano kutakuwa na uchaguzi na uzuri wa Katiba ya Zanzibar jambo lolote la kubadili lazima uitishe kura ya maoni na gharama zake ni sawa na uchaguzi mkuu.

Alisema ni vyema CCM ikakemea kauli za viongozi kama hao.

**KATIBA YA CCM**

Kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya mwaka 1977, Ibara ya 114 (1) inasema: "Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM wawili watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti anayeishi na kufanya kazi zake Tanzania Bara na Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM anayeishi na kufanyakazi zake Zanzibar, isipokuwa kwamba kuishi kwao hivyo hakutapangua upeo wa madaraka yao ya kushughulikia kazi za CCM, kwa Tanzania nzima.

Kifungu cha 2, "Makamu Mwenyekiti wa CCM atakuwa madarakani kwa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

**KATIBA YA ZANZIBAR**

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 toleo la 2010, ibara ya 28 kifungu cha 2 (a na b) "Kufuatana na maelezo ya kijifungu (1) cha kifungu hiki, Rais ataacha madaraka yake baada ya kumalizika miaka mitano kuanzia tarehe, ambapo: (a) kama yeye ni mtu ambaye ndiye mara ya kwanza amechaguliwa kuwa Rais chini ya Katiba hii alipokula kiapo cha uaminifu na kiapo cha kuwa Rais.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian




Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, akizungumza na makundi ya kinamama, vijana na makundi maalumu (hayapo pichani) wakati baraza hilo lilipoifikisha programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) katika Mkoa wa Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WET**

# Serikali kukutana na w'biashara Kariakoo leo

**Na Waandishi Wetu**

VUGUVUGU la tishio la mgomo wa wafanyabiashara lililotikisa kwa siku mbili kwenye mitandao ya kijamii limetulizwa baada ya serikali kukubali kupokea hoja zao na kukutana nao leo jijini Dodoma.

Jana, wafanyabiashara Kariakoo walisambaza kipeperushi chenye ujumbe wa kuhamasisha mgomo kufanyika leo na kwamba hakuna duka litakalofunguliwa eneo la Kariakoo na yeyote atakayeonekana amefungua atashughulikiwa.

"Wafanyabiashara wote wa Kariakoo mnatakiwa kufunga biashara zenu zote yakiwamo maduka na ofisi na chochote unachokifanya kuanzia Jumatatu Juni 24 bila ukomo hadi pale changamoto zetu zote za kibiashara zitakapotatuliwa," lilisema tangazo hilo.

Tangazo hilo lilisema wafanyabiashara wa mikoa ya Mbeya, Iringa, Mwanza, Arusha, Ruvuma, Kagera na Rukwa wanatakiwa kuanza mgomo huo kuanzia Jumanne Juni 25, bila ukomo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, alisema eneo hilo liliingia kwenye sintofahamu baada ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuingiza timu za vijana ukaguzi wa mizigo.

"Moja, Kariakoo ni soko ambalo upande wa kushoto kuna machinga, kulia machinga, mbele machinga na ndani ndio mmiliki wa duka, machinga anauza bila risiti, lakini bidhaa ni ile ile anayouza mfanyabiashara aliyepo dukani.

"Pili, sasa mizigo mingi inayoingai Kariakoo ni 'consolidated' inakuja mizigo ya vifurushi vidogo vidogo ambavyo TRA wameshindwa kukadiria kodi kwa asilimia 100, wanatoa kwenye kasha zima, wanaweza kukadiria Sh. milioni 40. Wafanyabishara wanapokwenda kugawana wanashindwa kupata risiti ya TRA kila mmoja.

Kwa mujibu wa Mbwana, usumbufu mwingine ni wanapoonyesha risiti wanaambiwa iko sawa, lakini haijawekwa TIN ya mteja.

Aidha, alisema jana alikutana na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na Kamati ya Bajeti ambaye aliahidi hadi leo atakuwa ametatua matatizo ya wafanyabiashara.

**TRA YAFUNGUKA**

Akizungumzia malalamiko ya wafanyabiashara hao, Kaimu Mkurugenzi wa Elimu na Mawasiliano kwa Mlipakodi wa TRA, Hudson Kamoga, alisema mpaka jana walikuwa hawajapokea malalamiko rasmi zaidi ya kuona taarifa hizo zilizosambaa mtandaoni.

Alisema upo mfumo rasmi wa kupokea malalamiko ya walipakodi na hushughulikiwa kwa utaratibu na hiyo ni haki yao kusikilizwa.

Kuhusu suala la kamata kamata, alisema mamlaka hiyo haina mahabusu wala polisi, ni jukumu lake kufanya ukaguzi na kuangalia mwenendo wa biashara kama sheria inavyotaka.

"Kutoa risiti kielektroniki si matakwa ya TRA, ni matakwa ya sheria ambayo mamlaka ni msimamizi wa hiyo sheria. Kila unaponunua dai risiti na kila unapouza toa risiti ili kuepushana na hizi vurugu.

Aidha, alisema kutoka mwaka 2021 mpaka sasa (2024) mapato TRA yanayokusanywa yameongezeka kwa kiwango kikubwa kwa sababu mianya ya ukusanyaji mapato imezibwa.

Kamoga alitoa wito kwa wafanyabiashara hao walioitishia kufunga maduka leo kwamba, kwa sasa wanaelekea mwisho wa mwaka wa fedha ambao ni mwisho wa kuwasilisha marejesho (returns), na mwisho wa kulipa kodi ya mapato ya awamu ya pili.

Alisema TRA inawataka walipe kodi kwa wakati na kwa hiari na kusisitiza kwamba, mamlaka hiyo haitumii mabavu kukusanya kodi.

**RC DAR AWAANGUKIA**

Jana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila aliingilia kati na kuwataka wafanyabiashara kuwa na subira wakati serikali ikifanyia kazi changamoto zao.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema wafanyabiashara hao wanaweza kuwa na malalamiko ya msingi, lakini njia wanayochagua ya kugoma haiko sawa.

Alisema serikali imekuwa ikikaa mara kwa mara na wafanyabiashara wa Kariakoo kusikiliza malalamiko yao na changamoto nyingi tayari zimeshaanza kufanyiwa kazi na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam.

"Wametangaza kwamba atakayefungua biashara watamshughulikia, lakini mimi naomba suala la mgomo lisiwe jambo la pamoja bali kila mtu atafakari vya kutosha kabla ya kuamua kufunga biashara natoa rai kwa wafanyabiashara kuacha kufuata mkumbo," alionya Chalamila.

Alisema baadhi ya malalamiko ya wafanyabiashara tayari yamepokewa na yanafanyiwa kazi na alikiri kuwa yapo ambayo yatachelewa kufanyiwa kazi yakiwamo masuala mtambuka yanayohusu sheria.

"Hata sisi watumishi wa umma tuna mambo yetu tunayotaka yafanyiwe kazi na serikali, lakini kuna namna bora ya kuyafikisha bila kusababisha taharuki kama hii inayotengenezwa Kariakoo," alisema Chalamila.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe, alizungumza na gazeti hili jana na kusema kuwa Jumuiya hiyo haijatangaza mgomo huo na badala yake ni kikundi cha wafanyabiashara wa eneo hilo.

Mei 17, mwaka 2023, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliunda kamati ya watu 14 ikiwa ni saba kutoka serikalini na saba Jumuiya ya Wafanyabiashara kwa ajili ya kushughulikia kero za kundi hilo na kupendekeza hatua stahiki za kuchukuliwa.

Hatua hiyo ilikuja baada ya wafanyabiashara kugoma kufungua biashara kwa siku kadhaa, hali iliyolazimu Waziri Mkuu akiwa ameambatana na mawaziri kwenda kuzungumza nao kwa kusikiliza kero za mmoja mmoja.

Hata hivyo, ripoti ya kamati hiyo haijawahi kuwekwa hadharani.

**Imeandikwa na Joseph Mwendapole na Romana Mallya**

# Rais TLS ataja chanzo mkwamo Katiba mpya

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Harold Sungusia, amesema moja ya chanzo kikubwa cha kuchelewesha mchakato wa upatikanaji wa Katiba mpya ni pamoja na mgongano wa maslahi.

Aidha, kikwazo hicho kimesababisha msimu uliopita kushindwa kufanyia kazi maoni kuhusu mchakato wa Katiba mpya, yaliyotolewa na wananchi pamoja na wadau mbalimbali.

Wakili Sungusia alisema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua mkutano wa wadau kutoa maoni yao kuhusu mchakato wa Katiba mpya.

Alisema safari hii TLS wamejipanga kuhakikisha maoni waliyochukua katika mikoa mitano yanafanyiwa kazi ili mchakato huo ukamilike.

Alibainisha mambo matatu ambayo wameyagundua kwa wananchi na baadhi ya viongozi kuhusu Katiba iliyopo sasa kwa mikoa ambayo wamefanya mikutano.

Kwa mujibu wa Wakili Sungusia, kuna makundi matatu ambayo ni; wanaosema "Katiba ya sasahivi haina tatizo lolote tusipoteze muda tuendelee na maisha yetu".

Kundi la pili ni wale wanaosema "Katiba iliyopo ina dosari kadhaa ambazo tunaweza kuzirekebisha tukaenda mbele" na kundi la tatu ni "wanaosema Katiba iliyopo haifai kabisa inahitajika katiba mpya ambayo itasaidia nchi kwenda mbele".

"Wananchi wana maoni mengi, lakini ukisikiliza kwa haraka utagundua kwamba wamesikitishwa na kilichotokea mwaka 2014 baada ya ile Tume ya Katiba iliyokuwa ikiongozwa na Jaji Joseph Warioba kumaliza kazi yake," alisema.

Aidha, miongoni mwa mambo ambayo wamejiuliza ni kwanini mchakato uliopita ulikwama.

"Usipojua ulipoangukia na kilichokusababisha ukaanguka, huwezi kuchukua tahadhari kwa hatua unazoenda mbele, tulikwama kwenye mchakato uliopita kwa sababu ya mgongano wa maslahi, waliokuwa nje ya utawala walidhani kwamba watatumia katiba kuweza kuingia madarakani na waliokuwa madarakani walidhani watatumia mchakato wa katiba kuendelea kubaki madarakani," alisema.

"Sisi tunataka Katiba ya wananchi sio Katiba ya makundi fulani katika nchi hapana, ni Katiba ya raia wote wajisikie Katiba ni ya kwao kwa utaratibu huo tunapendekeza mchakato utakaofuata wakupata katiba ya wananchi usimamie umahiri wake," alisema.

Pia, watakaohusika katika kuandaa mchakato wa katiba wasihusike katika kugombea nafasi zozote za kisiasa.

**MAUAJI WENYE UALBINO**

Katika hatua nyingine, Wakili Sungusia alizungumzia suala la mauji ya watu wenye ualbino yanayoendelea nchini amesema kuwa TLS inakemea kwa nguvu zote.

Alisisitiza kuwa kamwe Watanzania wasikubali jambo hilo liendelee na kutoa wito kwa taasisi zote kuchukua hatua kukemea hayo mauaji.

Inock Isaya, akizungumza katika mjadala huo, alisema kuwa Katiba itakayopendekezwa iwazingatie watu wote wenye ulemavu wa aina tofauti.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la John Hopkins Centre for Communication Programs, Waziri Nyoni, akiwasilisha mada kuhusu kampeni ya Holela-Holela Itakukosti kwenye mkutano wa Mawaziri wa Afya kutoka nchi tisa za ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Arusha, walikubaliana kuongeza nguvu zaidi katika kukabiliana na usugu wa dawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya milioni 10 hufariki dunia kwa usugu wa dawa

**Na Gwamaka Alipipi**

WATU zaidi ya milioni 10 duniani wanafariki dunia kila mwaka kutokana na tatizo la Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa (UVIDA), huku nusu ya vifo hivyo vikitokea nchi za Afrika.

Kutokana na hali hiyo, mawaziri wa afya kutoka nchi tisa za Afrika (Ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika) wamefanya mkutano jijini Arusha mwishoni mwa wiki na kukubaliana kuongeza nguvu kukabiliana na tatizo hilo, ikiwamo ongezeko la bajeti na nyenzo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Afya ya Ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (ECSA-HC), Profesa Yoswa Dambisya, alisema tatizo la UVIDA linatarajiwa pia kuathiri zaidi ya asilimia 3.5 ya pato la kila taifa ifikapo mwaka 2050.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema tatizo la UVIDA linasababisha wagonjwa kutumia siku nyingi hospitalini wakati wakipatiwa tiba, kwa sababu ni vigumu kutibu magonjwa ambayo hayasikii dawa.

"Gharama za matibabu zinakuwa juu na pale ambapo dawa zitashindwa kabisa kufanya kazi, basi vifo hutokea," alisema Waziri Ummy.

Mawaziri kutoka Lesotho na Uganda walisema tatizo kubwa la UVIDA katika nchi zao linawapata hasa wagonjwa wa kifua kikuu ambao huwa wanashindwa kutimiza tiba kwa kuacha matumizi ya dawa katikati kunakosababishwa na umaskini.

Waziri wa Afya wa Uganda, Dk. Jane Ruth Aceng, alisema: "Dawa za tiba ya kifua kikuu ni gharama, kwa hiyo wananchi wanashindwa kutimiza tiba yote na hivyo kusababisha vimelea vya ugonjwa hua kujenga usugu dhidi ya maradhi."

Zaidi ya watu milioni tano wanafariki dunia kila mwaka katika Ukanda wa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na tatizo la UVIDA.

Kutokana na kupambana na hali hiyo, hivi karibuni Tanzania ilizindua kampeni dhidi ya matumizi mabaya ya dawa za tiba iitwayo 'Holela-Holela Itakukosti' ikiwa na maana ya 'uzembe unagharimu', inayoonyesha uhusiano muhimu kati ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira.

Kampeni hiyo inalenga kushughulikia sababu mbalimbali za kijamii zinazosababisha tatizo la UVIDA na magonjwa ambayo yanaweza kuambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Pia, kampeni hiyo ilizinduliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Makamu Rais (Mazingira) na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa Breakthrough Action.

# Uchumi kidijiti kukua kumaliza changamoto

**Na Maulid Mmbaga**

UCHUMI wa kidijiti unatarajiwa kukua zaidi nchini pamoja na kumaliza changamoto ya kukosekana kwa huduma ya intaneti kutokana na kukatika kwa mkongo wa baharini, baada ya wadau wa teknolojia na mawasiliano kuanza kutumia mkongo mpya wenye uwezo mara 10 ya uliokuwapo.

Hatua hiyo inatarajiwa baada ya wadau hao ikiwamo Airtel Tanzania kuanza kutumia rasmi mkongo wa mawasiliano unaopita baharini wa 2Africa unaounganisha mabara matatu, jambo linalotarajiwa kuleta maendeleo katika kupanua na kuimarisha miundombinu ya kidijitali Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Airtel jana, mkongo huo utaiweka Tanzania katika viwango vya juu vya mabadiliko ya kukua kwa huduma za kidijitali na kukidhi mahitaji ya uchumi wa nchi, pamoja na kusaidia kuanzishwa kwa vituo vya kuhifadhi kumbukumbu kielektroniki ili kukidhi ongezeko la shughuli za kidijitali nchini.

"Mkongo wa 2Africa sasa umeanza rasmi kuhudumia kampuni za teknolojia ambazo sasa zinapokea masafa ya uwezo wanaohitaji kupitia kituo cha Airtel Cable Landing Station kilichozinduliwa siku chache zilizopita na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Uzinduzi wa mkongo huo umekuja wakati muafaka, hasa kutokana na kukatika kwa nyaya za mkongo wa mawasiliano unaopita chini ya bahari hivi karibuni ambazo ziliathiri baadhi ya maeneo ya Afrika Mashariki, ikiwamo Tanzania," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Iliongeza kuwa mkongo huo unaiunganisha Tanzania na maeneo 43 duniani, na inahudumia zaidi ya watu bilioni tatu na kukuza muunganiko wa kimataifa wa wafanyabiashara kidijitali.

Katika uzinduzi huo siku chache zilizopita Rais Samia alisema Mkongo huo unaunga mkono mipango ya Wizara ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari, ikiwamo ya maabara ya akili mnemba na roboti.

"Miundombinu hii sio tu italeta mapinduzi katika huduma za mawasiliano, lakini pia itaharakisha ukuaji wa uchumi kwa kuimarisha muungano na mataifa mengine," Rais Samia alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Airtel, Dinesh Balsingh, alisema mazingira wezeshi ya serikali pamoja na uwepo wa mfumo bora wa udhibiti ndio sababu zilizowawezesha kuzindua kituo hicho kabla ya nchi nyingine.

"Ujio na uwepo wa mkongo huu wa mawasiliano umefanikiwa kuwa nchini kutokana na maono ya uongozi wa Rais Samia na Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye. Pia unaifanya Tanzania kuwa kitovu na lango la kusambaza huduma kidijitali kimataifa, kukuza fursa za kiuchumi na maendeleo ya kiteknolojia," alisema Balsingh.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alisema kuwa mkongo huo utachochea na kuboresha zaidi huduma bora za intaneti nchini.

"Mkongo huu mpya utakuwa msaada mkubwa katika kukabiliana na mahitaji ya huduma za mtandao wa intaneti nchini, ambazo mahitaji yake yamekuwa yakiongezeka maradufu kila baada ya miaka miwili.

"Nina hakika kuwa teknolojia hii itasaidia utekelezaji wa haraka wa mkakati wetu wa kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika sekta zote na kuboresha uchumi wa kidijitali ambao Tanzania inatamani kufikia," alisema Dk. Bakari.

Waziri Nape alisema uwapo wa mkongo utasaidia kuunganisha nchi kimataifa na kuwepo kwa mifumo ya kibunifu kidijitali ikiwemo kuunganisha mifumo mbalimbali ya serikali kuwa jumuishi.

Kwamujibu wa makadirio ya 'RTI International' Mkongo wa 2Africa unatarajiwa kuzalisha kati ya dola bilioni 26.4 hadi 36.9 ikiwa ni matokeo ya ukuaji kiuchumi kutokana na huduma zitakazotolewa na mkongo huo barani Afrika ndani ya miaka ya awali.

# Uvutiaji mitaji viwanda EPZA wazidi kupaa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Eneo Huru la Uwekezaji kwa Mauzo Nje (EPZA), imesema imevutia mtaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani zaidi ya bilioni mbili (zaidi Sh. trilioni 5.3) katika kipindi cha miaka 10.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya EPZA, Charles Itembe, alisema mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya siku tatu ya Rais wa Guinea Bissau, Umaro Sissoco Embaló ambaye alipata fursa ya kutembelea eneo Maalum la Uwekezaji la Benjamin William Mkapa (BWM-SEZ), Mabibo jijini Dar es Salaam.

Itembe alisema kuwa mauzo nje ya nchi katika kipindi hiki yalifikia Dola za Kimarekani zaidi ya bilioni 2.5 (zaidi Sh. trilioni 6.5).

"Mafanikio haya ya kuvutia mitaji na mauzo nje ya nchi yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za serikali katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji hivyo kuvutia wawekezaji wengi nchini," alisema.

Alisema katika kipindi hiki, EPZA ilisajili zaidi ya viwanda 250 kwenye sekta mbalimbali ambavyo vimetengeneza ajira za moja kwa moja zaidi ya 60,000 na zisizo za moja kwa moja zaidi ya 100,000 kwenye sekta za kilimo, uchakataji wa madini, vifungashio, nyama na bidhaa za miti.

Kati ya viwanda alivyotembelea Rais wa Guinea Bissau ni cha Tanzania Tooku Garment ambacho huuza bidhaa zake nchini Marekani.

Rais wa Guinea Bissau alionesha kufurahishwa na namna viwanda vinavyofanya kazi kwa ufanisi mkubwa huku akitoa ujumbe kuwa Bara la Afrika litafanikiwa kujenga uchumi imara wa viwanda kupitia programu za EPZ na SEZ. Itembe alimwambia Rais huyo kuwa eneo la BWM-SEZ lina miundombinu ya majengo 21 ambayo yana viwanda mbalimbali vinavyozalisha bidhaa mbalimbali na kuajiri zaidi ya Watanzania 4,500 kwa ajira za moja kwa moja na ajira zisizo za moja kwa moja 8,600.

Pia, eneo la BWM-SEZ limevutia mitaji yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 51.9 na mauzo nje ya nchi yenye thamani ya Dola milioni 82.9 katika sekta za uchakataji wa mazao ya kilimo, kadi maalum za kielektroniki, kahawa na nguo. Alisema kuwa EPZA imejikita katika kutengeneza maeneo huru ya kiuchumi ili kuvutia uwekezaji kutoka sekta za umma na binafsi.

Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa programu hizi za SEZ na EPZ zinafanikiwa ili kuvutia uwekezaji mkubwa zaidi na kuchangia ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Alisema EPZA inatoa fursa na vivutio mbalimbali kwa wawekezaji ambavyo vinawahakikishia usalama wa mitaji yao na kupata faidi kutokana na uwekezaji huo.

Mfano ni juhudi za serikali katika kuendeleza maeneo ya SEZ ni mradi wa BWM-SEZ kutokana na viwanda mbalimbali kuanzishwa na kujengwa na kufanya mchango mkubwa katika uchumi wa viwanda.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ratiba ya Ligi Kuu itoke mapema timu zijipange

**HIVI** majuzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Almasi Kasongo, alisema wameshaanza kutengeneza ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara ya msimu ujao.

Akaongeza kuwa msimu ujao wanatarajia kutengeneza ratiba bora zaidi ambayo itakuwa na uzani sawa kwa klabu zote na zitawapa muda makocha na wachezaji kujiandaa, kupata muda wa kufanya mazoezi na kusafiri kwenda vituoni kwa wakati.

Tunaipongeza Bodi ya Ligi kwa kuliangalia hilo, kwani msimu uliopita kulikuwa na baadhi ya timu zinacheza mechi mbili baada ya siku tatu, kitu ambacho ni hatari kwa afya ya wachezaji, lakini hushusha ushindani.

Tunatamani kuona angalau ratiba hiyo inatoa nafasi kwa timu kucheza mechi mbili kwa wiki ama moja, ili kutoa muda wa wachezaji kupumzika, na pia makocha kupata nafasi ya kuvitengeneza vikosi vyao na kuondoa mapungufu ambayo wameyaona.

Msimu uliopita baadhi ya makocha walikuwa wakilalamika kutokuwa na muda wa kurekebisha mapungufu kwa sababu ya kubanwa na ratiba, matokeo yake timu ikicheza mechi hii, inakwenda kucheza nyingine bila kufanya maandalizi yoyote kwa sababu muda mfupi wanaoupata wanautumia kwa safari.

Hata kama kila siku kuanzia Jumatatu hadi Jumapili kutakuwa na mechi ya Ligi Kuu, lakini TPLB inatakiwa kutazama timu itakayocheza siku husika kuipa angalau siku tatu kabla ya kucheza mechi nyingine.

Tukiachana na hilo ambalo Bodi wanasema watalifanyia kazi, kuna suala la kutangazwa kwa ratiba mpya.

Tumekuwa tukishuhudia wakati mwingine ratiba ikitangazwa wiki mbili tu kabla ya ligi kuanza. Hii si sahihi hata kidogo. Bodi ya Ligi ijitahidi ratiba ya msimu mpya itoke angau mwezi mmoja kabla ya kuanza na hilo linawezekana.

Tumeona tayari ratiba ya Ligi Kuu England itakayoanza Agosti 16, mwaka huu imetoka kabla hata ya Julai.

Ni kwamba siku ya ufunguzu, Machester United itacheza dhidi ya Fulham na Agosti 17, michezo sita itachezwa.

Yaani Chama cha Soka nchini humo kimetoa ratiba ya msimu mpya, kabla hata wachezaji hawajaanza maandalizi ya msimu mpya (pre season), kwani ndiyo kwanza wako mapumziko.

Hivyo makocha na wachezaji wataanza maandalizi wakiwa wanafahamu mechi ya kwanza watacheza na timu gani, na zinazofuata, hivyo kuwa na nafasi ya kujiandaa kutokana na aina ya mpinzani wanaokwenda kukutana nao.

Mfano, tayari Fulham wanafahamu watafungua na Manchester United, kwa hiyo wameshajua watakwenda kuwakabili vipi. Makocha kufahamu aina ya timu wanazokwenda kukutana nazo mapema kunawapa muda wa kutengeneza mifumo ya kukabiliana nao, kwani kila timu ina staili yake ya uchezaji.

Huku kwetu inawezekana mpaka timu zinaanza 'pre season' zitakuwa hazijui zitaanza na nani na wapi, hivyo tunaikumbusha TPLB kulimulika hilo kwa kuhakikisha ratiba hiyo inatoka mapema.


Ifike wakati bodi hiyo kubadilika na kuanza kutoa ratiba mapema, hata ili timu zipate kujiandaa vema jambo ambalo litaongeza ushindani katika ligi yetu.

Inawezekana kuwa hivyo kwa sababu Kalenda ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (CAF), imeshatoka, ambapo mechi za awali za Ligi ya Mabingwa na Shirikisho, zinaanza Agosti na Oktoba mpaka Desemba na hatua za makundi, mtoano hadi fainali itakuwa Machi hadi Mei mwakani.

Hivyo Nipashe tunashauri na ratiba ya Ligi Kuu kutoka mapema kwani itazipa nafasi timu kujiandaa na mpinzani wanaokwenda kukutana naye, kuandaa mipango ya usafiri pamoja na kufahamu aina ya viwanja ambavyo watakwenda kuvitumia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Klabu zifuate kanuni, weledi kwenye usajili

Na Faustine Feliciane

**DIRISHA** la usajili kwa klabu za Ligi Kuu, Championship, First League na Ligi ya Wanawake limefunguliwa rasmi Juni 15 na linatarajiwa kufungwa Julai 15, mwaka huu.

Huu ni wakati wa klabu kufanya usajili kwa ajili ya kuviimarisha vikosi vyao kuelekea kwenye msimu mpya wa 2024/2025.

Usajili mzuri kwa kila klabu hakuna shaka kutatengeneza ushindani mkubwa kwa timu shiriki na hivyo kuifanya ligi kuwa bora na yenye ushindani mkubwa.

Hata hivyo, ili mambo yote yaende sawa ni lazima klabu zifuate utaratibu kwenye mchakato wa usajili wanaoufanya.

Binafsi, ninaona hipo haja ya kuzikumbusha klabu zetu kufuata utaratibu na makubaliano kwa sababu siku chache zilizopita baada ya dirisha la usajili kufunguliwa tayari zimeanza kuonekana sarakasi kwenye usajili kwa baadhi ya klabu hapa nchini.

Baadhi ya klabu hizi ni pamoja na Simba na Coastal Union ya Tanga juu ya mchezaji Lameck Lawi.

Mchezaji huyu ameteka dirisha la usajili mwanzoni tu kutokana na namna alivyosajiliwa kutoka Coastal Union kwenda Simba.

Siku chache baada ya Simba kupitia Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, kumtangaza mchezaji huyo kuwa ni wao tayari baada ya kukamilisha dili la usajili.

Baadaye uongozi wa Coastal Union ulitoka hadharani na kukanusha vikali kukubaliana na Simba juu ya mchezaji huyo.

Msemaji wa klabu hiyo, Abas Elsabri, alisema wazi kuwa Simba wamekiuka makubaliano yao ya awali kuhusu usajili wa mchezaji huyo, hivyo Lawi ataendelea kuwa mchezaji wao.

Simba kwa uhakika wakajibu mapigo kwa kusisitiza kuwa wamemalizana na mchezaji huyo na tayari wamemlipa pesa zake za usajili, lakini pia walimaliza kuwalipa Coastal Union, hivyo mchezaji huyo ni mali yao.

**Baadhi ya klabu hizi ni pamoja na Simba na Coastal Union ya Tanga juu ya mchezaji Lameck Lawi. Mchezaji huyu ameteka dirisha la usajili mwanzoni tu kutokana na namna alivyosajiliwa kutoka Coastal Union kwenda Simba.**

Mivutano kama hii haina afya kwa soka letu, ni vema klabu zikubaliane kwa utaratibu waliojiwekea na ziache kutunishiana misuli kwa mustakabali wa mpira wetu, lakini kwa mchezaji husika.

Ni vema viongozi wa klabu hizo kukaa pamoja na kujadiliana ili wafikie mwafaka mapema.

Hakuna kitu kinachoshindikana kwenye mazungumzo, Simba, Coastal Union wakae pamoja watatue mgogoro huu ili mchezaji husika awe kwenye nafasi nzuri ya kuendeleza kipaji chake.

Simba tayari wametangaza kupambana mpaka mwisho na ikiwezekana kulipeleka suala hilo Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), kama mchezaji huyo hataidhinishwa kuichezea timu yao msimu ujao.

Binafsi, naona hakuna haja ya kufanya hivyo, bado kuna nafasi ya klabu hizi mbili kukaa pamoja na kujadiliana ili kufikia mwafaka kabla ya kushtakiana FIFA au hata Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Inaelezwa Coastal Union wamezirudisha fedha za Simba za usajili, lakini je, vipi kuhusu mchezaji husika ambaye tayari ameshamalizana na klabu hiyo kwa ajili ya kujiunga nayo kwenye dirisha hili la usajili?

Busara ni muhimu kutumika kwenye jambo hili, nashauri Simba na Coastal zikae pamoja na kuacha kumweka kwenye wakati mgumu mchezaji husika.

Na huu uwe mfano kwa klabu nyingine kufuata kanuni na weledi kwenye usajili katika kipindi hiki ili kuepuka migogoro na mivutano.

## HABARI KITAIFA

# CCM, CPC vyakubaliana kuimarisha uhusiano

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), vimekubaliana kuimarisha zaidi uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia kwa manufaa ya mataifa hayo mawili.

Makubaliano hayo yamefikiwa mwishoni mwa wiki kupitia kikao baina ya Katibu Mkuu CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi na Mjumbe Kamati Kuu ya CPC, Tang Dengjie, katika ofisi ndogo za CCM Lumumba jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho kilichoashiria tukio muhimu wakati wa ziara rasmi ya siku tatu ya Dengjie nchini Tanzania, Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Nchimbi, alisisitiza uhusiano wa kudumu na wenye manufaa kwa pande zote mbili kati ya CCM na CPC.

Balozi Dk. Nchimbi alisisitiza kuwa urafiki wa muda mrefu kati ya Tanzania na China, unaochagizwa na uongozi wa CCM na CPC, umeimarika zaidi ya miongo sita ya uhusiano wa kidiplomasia.

Alizungumzia pia kanuni za kiitikadi, kisiasa, kiuchumi na kijamii zinazoongoza ushirikiano huo, akibainisha jukumu lake ni mfano wa kuigwa kwa Afrika na dunia.

"CCM na CPC vina urafiki wa kindugu ambao umebadilika na kuwa msingi imara wa kukuza fursa za kiuchumi na uwekezaji unaolenga kuimarisha ustawi wa wananchi wetu," alisema Balozi Dk. Nchimbi.

Aidha, alisema uhusiano huo ulianzishwa na waasisi wa mataifa hayo, Mwalimu Julius Nyerere na Mwenyekiti Mao Zedong, na tangu wakati huo umekua na ushirikiano wa kimkakati.

Balozi Dk. Nchimbi alitambua jukumu muhimu lililofanywa na mazungumzo ya hivi karibuni ya ngazi ya juu, ikiwa ni pamoja na ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini China mwaka 2022, uhusiano kati ya nchi hizo mbili ulipandishwa hadhi na kuwa na ushirikiano wa kimkakati.

Alisisitiza kwamba ni ushirikiano uliofanikiwa katika sekta tofauti za ujenzi, afya, utalii, kilimo, dawa, biashara na uchumi na kuhimiza nchi hiyo kuendelea kuunga mkono uwekezaji katika sekta zinazoendelea Tanzania.

Tang Dengjie, alithibitisha dhamira ya China ya kuimarisha uhusiano wa pande hizo mbili na kuunga mkono mipango ambayo inanufaisha wakazi wa mataifa yote mawili.

Alisema miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya China na Tanzania ni ushahidi wa urafiki wa kudumu na kuheshimiana na wamejitolea kuimarisha zaidi uhusiano huo kwa manufaa ya watu.

Viongozi hao walielezea ushirikiano thabiti wa kiuchumi kati ya China na Tanzania, huku China ikiwa mshirika mkuu wa biashara wa Tanzania kwa miaka minane mfululizo.

Mwaka 2023, kiasi cha biashara baina ya nchi hizi kilifikia Dola bilioni 8.78, ikionyesha ongezeko la asilimia 5.66 kutoka mwaka uliopita.

China imewekeza kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania, ikiwa na takriban miradi 260 katika sekta mbalimbali, na hivyo kuimarisha nafasi yake ya kuwa mwekezaji mkubwa wa kigeni wa Tanzania.

Muktadha wa kihistoria wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ni ishara ya urafiki wa kudumu kati ya China na Afrika.



Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, akiendesha mjadala kwa wanafunzi wa shule mbalimbali kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Msimamizi uchaguzi asiwe aliyewahi kuwa kiongozi kisiasa'

**Na Christina Mwakangale**

MTUMISHI wa umma mwandamizi ni miongoni mwa waliotajwa kuwa na sifa za kuteuliwa kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi, isipokuwa kwa ambaye amewahi kuwa kiongozi wa kisiasa na kutiwa hatiani.

Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024, kuhusu uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine, iliyotungwa na Bunge, iliyosainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Machi mwaka huu, imeainisha masharti hayo ya kusimamia uchaguzi.

Sura ya kwanza ya sheria hiyo, sehemu ya sita, kifungu cha kwanza hadi saba, kimefafanuliwa mambo kadhaa kisheria, kifungu cha (3) na kifungu kidogo cha (2) mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi;

Endapo katika miaka mitano kabla ya uchaguzi husika (a) hajawahi kutiwa hatiani katika shauri la nidhamu au kosa lolote la jinai na kuadhibiwa kwa kifungo kinachozidi miezi sita;


Pia kifungu (b) kinasema hajawahi kuwa kiongozi wa chama cha siasa. Tume itatangaza majina ya watu walioteuliwa kuwa wasimamizi wa uchaguzi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa notisi itakayochapishwa na Gazeti la Serikali.

Kadhalika sheria hiyo, inaeleza (5); Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria hii, Tume inaweza kumteua mtu yeyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanayohusiana na mchakato wa uchaguzi.

Sehemu ya (6); Msimamizi wa uchaguzi, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 76 na maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, anaweza kuteua watendaji kwa idadi inayohitajika kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata.

Pia sehemu (7); Kila msimamizi wa uchaguzi na msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo, ataapa kiapo cha kutunza siri na kutoa tamko la kujitoa au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa, mbele ya Hakimu kwa kutumia fomu itakayoainishwa.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Taka zinazozalishwa na wafanyabiashara wadogo katika kituo cha daladala na Bajaj, Mbezi Luis Dar es Salaam, zikiwa zimerundikwa pembeni mwa kituo hicho jana, zina zaidi ya siku tatu bila kuondolewa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kinachokwamisha wanawake kugombea uongozi chatajwa

**Na Kulwa Mzee**

WAZIRI wa zamani na Mwenyekiti wa Taifa wa Wanawake wa Kiislamu Tanzania Bara, Shamim Khan, ametaja sababu tano zinazokwamisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ikiwamo uthubutu, matusi na rushwa ya ngono.

Alibainisha hayo jana katika ziara ya siku mbili ya furaha kwa Mama na Binti iliyoandaliwa na Kituo cha Utamaduni cha Jamhuri ya Kiislamu ya Iran na Ubalozi wa Iran Tanzania, mgeni rasmi akiwa mke wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda.

Shamim alihamasisha wanawake kujitahidi kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali badala ya kuwa wapigakura.

"Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa kura, lakini bado hatujitokezi. Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji. Juhudi zifanyike wafikiwe.

"Sababu ya tatu, rushwa ya ngono ni kikwazo, wanaume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," alisema.

Alisema mwanamke akitaka kugombea anapaswa kukataa rushwa ya ngono na anapokuwa na heshima hakuna atakayemfuata kwa hilo.

Shamim alitaja sababu ya nne kuwa ni kutojua kanuni za vyama na kutaka vyama vya siasa vifanye bidii kuzipeleka hadi ngazi ya chini ili kupata wanawake wengi.

Alisema sababu nyingine ni matusi ya nguoni ambayo hukimbiza kundi hilo kuingia kugombea nafasi mbalimbali.

Aidha, aliwaasa vijana kubadilika kwa kuacha kutumia vilevi kwa kuwa ni moja ya sababu inayowaingiza katika kufanya vitendo vya kikatili ikiwamo kuua wazazi wao kwa ajili ya mali.

"Mnatakiwa kuwaheshimu mama zenu. Zipo kesi nyingi za watoto kuwavunjia heshima mama zao. Mama ni pepo, pepo ya mtoto iko chini ya nyayo ya mama yake," alikumbusha.

Akitoa maoni yake kuhusu viti maalum vya udiwani na ubunge, Shamimu alisema, "vyama viweke ukomo wa miaka kumi baada ya hapo waingie kugombea wapigiwe kura. Siyo miaka yote sura zilezile, vijana watapata wapi nafasi," alihoji.

# TLP yatembeza bakuli uchaguzi kumrithi Mrema

**Na Sabato Kasika**

SIKU chache kabla ya uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), chama hicho, kimeomba mchango wa fedha kutoka kwa wadau wa mageuzi, kufanikisha uchaguzi huo.

Uchaguzi huo unatarajia kufanyika jijini Dar es Salaam, Juni 29, mwaka huu, ili kuziba nafasi hiyo iliyokuwa inashikiliwa na Hayati Augustine Mrema.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Makamu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Dominatha Rwechungura, alisema, ingawa maandalizi ya uchaguzi yanaendelea vizuri, bado wanahitaji kushikwa mkono.

"Bado tunaendelea kuwaombea wadau wa mageuzi kutuchangia fedha kwa ajili ya uchaguzi huu, tuna upungufu kidogo ingawa hayawezi kuathiri uchaguzi," alisema Dominatha. Alisema, ombi hilo la mchango wanalifikisha pia kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa ni mwana mageuzi na mpenda demokrasia, na wanaamini atawaunga mkono kwa chochote.

Aidha, aliwataja wanaowania nafasi hiyo kuwa ni, Richard Lyimo ambaye kwa sasa ni katibu.

"Wengine ni Mhandisi Aivan Maganza ambaye ni mwenyekiti wa vijana wa TLP Taifa, Stanley Ndamugoba, Kinanzaro Mwanga na Abuu Changaa," alisema.

Kwa zaidi ya mwaka mmoja tangu kifo cha Mrema, chama hicho kimekuwa kikiahirisha uchaguzi wa mwenyekiti, kutokana na sababu ikiwamo wagombea kufanyiana figisu.

Mrema alifariki dunia mwishoni wa Agosti mwaka 2022, kisha akachaguliwa Hamad Mkadam kuwa kaimu mwenyekiti wa chama. Hata hivyo, uchaguzi umekuwa ukipangwa na kuahirishwa na kusababisha malumbano hadi kufikia baadhi yao kutishia kufukuzana ndani ya chama.

IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE
AT ONE STOP CENTRE

MATRIMONIAL CAUSE NO. 11909 OF 2024
STEPHEN KAGARUKI MUTALEMWA PETITIONER
VERSUS
HELLEN DALALI NANGAJU RESPONDENT

NOTICE OF EXPARTE JUDGMENT

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for Ex-parte Judgment on 25th day of JUNE 2024 at 08:30 PM Before HON: MWAFIRI

Your required to appear in this Court without Failure.

GIVEN under my hand and Seal of the Court this 14th, JUNE 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

COPY TO BE SERVED UPON
HELLEN DALALI NANKAJU

# Kisarawe kuja kivingine kimaendeleo

**Na Julieth Mkireri,**
KISARAWE

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, amemwahidi Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kubadilisha wilaya hiyo kimaendeleo kwa kusimamia miradi iliyolengwa kutekelezwa kwa wakati.

Magoti ameyasema hayo mwishoni mwa wiki aliposhiriki kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani kujadili hoja za Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kilichofanyika mjini humo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa.

Magoti alisema atahakikisha kila Mtendaji anatekeleza majukumu yake ya kusimamia miradi ya maendeleo inakamilika kama ilivyolengwa.

Akiwa katika Baraza hilo Magoti alisema ili kuondoa uzembe kwenye miradi kila mkuu wa idara atakuwa na wajibu wa kusimamia majukumu yake ipasavyo kwa kuwajibika kwenye eneo lake.

"Mkuu wa mkoa wiki ijayo hapa tutakuwa na kikao na wakuu wa idara na kila mmoja ataeleza mwaka wa fedha unaoisha amefanya nini na mipango yake kwa mwaka ujao ni ipi," alisema Magoti. Pia alisema anatarajia kufanya ziara hivi karibuni kwenye kata zote za wilaya hiyo na amewapongeza madiwani kwa kazi wanazofanya kwa kushirikiana na serikali kuondoa vikwazo kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, alisema halmashauri hiyo inatakiwa kupanga vipaumbele kufanya matumizi kulingana na bajeti.

Kunenge pia aliwaelekeza watendaji kuzuia hoja zisitokee na kumaliza ambazo hazijafungwa kwa kuzingatia maelekezo.

Aliagiza kuanzia sasa kila mkuu wa idara anatakiwa kuwajibika kuwasilisha hoja zake mwenyewe badala ya kumwachia Mkurugenzi pekee wakati uzalishaji unatoka kwenye idara.

Naye Mkaguzi wa nje Mkoa wa Pwani toka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, CPA Pastory Masawe, alisema halmashauri hiyo inatakiwa kujikita kuzuia kuzalisha hoja mpya na pia kukusanya zaidi mapato na kuwa makini kwenye matumizi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kisarawe, Beatrice Dominic, kwa kushirikiana, na watendaji wanaendelea kufunga hoja ambazo zimewasilishwa na kudhibiti uzalishaji wa hoja mpya.



# Kikwazo wanawake kutwaa uenyekiti vijiji, vitongoji chatajwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI wanawake wa pembezoni mwa nchini wakipambana na kuvunja mwiko wa nafasi za uenyeviti wa vijiji na vitongoji kushikwa na wanaume, wanaharakati wameeleza bado kundi hilo halijaweza kuingia katika mchakato huo kwa wingi kwa sababu ya kusukumwa kwenye viti maalum.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la kiraia la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, alisema wanatamani kuwepo ongezeko la wanawake kwenye uchaguzi wa mwaka huu wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, kwa kuwa sera ya viti maalum inawanyima wengi kuwa na sauti.

Akizungumza mwishoni mwa wiki iliyopita na wanawake vinara wa uhamasishaji kuingia katika mchakato huo kutoka Wilaya za Siha na Moshi, Rutazaa alisema:

"Vile viti maalum vinakuwa ni viti vya kuweka wanawake kule kama alama ya kuwapo kwenye uchaguzi na vyombo vya uamuzi, lakini unakuta ile nguvu yao ya kuweza kuongea hoja, na lile kundi analolitetea inakuwa ni ndogo," alisema na kuongeza kuwa:

"TUSONGE tunaona kwa sheria zilizopitishwa na Bunge na kusainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kama zitatumika ipasavyo, zitakuwa zinapunguza kwa kiasi kikubwa yale machungu ya yale maeneo ambayo yanaonekana kwamba yana changamoto."

Alisema TUSONGE kama wanaharakati wa maendeleo ya jamii hasa kwenye eneo la wanawake, wanatamani ongezeko la wanawake kwenye uchaguzi huo na mkuu mwakani.

"Tunatamani hilo kwa sababu kwa kiasi kikubwa unakuta kina mama wengi bado hawajaweza kuingia katika huu mchakato wa uchaguzi, kwa sababu mara nyingi wamesukumwa kuingia kwenye vile viti vinavyoita viti maalum," alisema.

Mary Laizer, Mkazi wa Kijiji cha Majengo Kata ya Biriri, Wilaya ya Siha, alisema kutokana na kazi kubwa inayofanywa na wanawake walioko katika uongozi kwa sasa, wanaume wametambua wanaweza kuongoza kwa asilimia kubwa.

"Kwa hiyo vita ya madaraka kati ya mwanaume na mwanamke itakuwa haina mashiko tena.

Lakini kama kuna kitu sitamani katika uchaguzi huo wa vijiji ni rushwa," alisema na kufafanua kuwa:

"Rushwa ndio kitu ambacho kwa sasa sitamani kitokee katika uchaguzi huu, kwa sababu wagombea wanawake watakandamizwa, na hasa wale ambao hawana kitu kama sisi."

Elizabeth Mmanga, Mkazi wa Kijiji cha Kahe Magharibi, Wilaya ya Moshi, alieleza kuwa uchaguzi huo unawapa picha kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa ya uongozi kutokana na elimu ambayo wanawake wanapata.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Buriani, akizungumza na madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni katika Baraza Maalumu la Madiwani la kupokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) juzi, halmashauri hiyo imepata hati safi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# RITA yajitosa kutatua mgogoro Taasisi ya Kiislamu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) imeunda tume kuchunguza mgogoro katika taasisi ya dini ya kiislamu ya Arusha Muslims Union unaodaiwa kusababishwa na baadhi ya waumini wake kutokana na ubadhirifu.

Akizungumza na waumini wa dini hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, alisema lengo la ujio wake ni kutatua mgogoro huo unaodaiwa kusababishwa na ubadhirifu wa mali za taasisi hiyo uliodumu kwa muda mrefu.

Alisema baada ya kupata taarifa kuwa bodi ya wadhamini wa taasisi hiyo inadaiwa kutafuna kiasi kikubwa cha mali za waumini, amefika kutatua mgogoro huo.

Kanyusi ambaye ni Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali, alisema katika kikao cha kwanza kati yake na wadhamini wa bodi hiyo na waumini na wanachama wa taasisi hiyo kilichofanyika Machi 14, mwaka huu, walibaini kuwa bodi ilikuwa ikifanyakazi kinyume cha sheria kwa kuwa muda wake ulikuwa umeisha.

"Katika kikao hicho tulibaini malalamiko ya wanachama yalikuwa na ukweli na bodi ya wadhamini muda wake, ulikuwa umekwisha na kukubaliana kuunda kamati ya mpito itakayokuwa na majukumu ya kufanya marekebisho ya katiba na kuitisha uchaguzi wa viongozi, pia kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya taasisi hiyo," alisema.

Alisema kamati ya mpito ilikabidhiwa majukumu mbalimbali ikiwamo kuandaa taarifa ya mapato na matumizi na kutoa taarifa yenye dosari.

Kanyusi, alisema taarifa hiyo ilimlazimu Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali kuunda tume mpya ya mpito kuchunguza mgogoro wa taasisi hiyo kwa muda wa siku 14 na kutoa majibu.

"Mimi kama Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria ya muunganiko wa bodi ya wadhamini, natakiwa kuunda kamati ya uchunguzi kujiridhisha zile tuhuma dhidi ya bodi ya wadhamini za kutumia vibaya mali za taasisi za ya Arusha Muslims Union zina ukweli na kuleta majibu," alisema.

Alisisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa watakaobainika kutumia vibaya mali za taasisi hiyo.

Alisema watahakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, huku wakijua kuwa mali hizo sio zao ni za wanachama.

# Upotevu wa maji wapata mwarobaini

**Na Jaliwason Jasson**, MANYARA

WANATAALUMA waliolelewa na kusomeshwa kwa ufadhili wa Shirika la Compassion International- Tanzania wamebuni mfumo wa kudhibiti upotevu wa maji yanayozalishwa na mamlaka za maji nchini.

Wamesema wako tayari kuisaidia serikali kutatua tatizo hilo la upotevu wa maji ambao umekuwa ukipigiwa kelele katika jamii.

Mwanafunzi wa Chuo cha Donbosco Technical Institute of Dodoma, anayetokea Klasta ya Kiteto, Abednego Wilfred, alisema aliguswa kutengeneza mfumo huo 'Automatic Pump' kudhibiti upotevu wa maji mitaani.

"Nimebuni huu mfumo baada ya kuona upotevu wa maji na watu wengi wanalalamikia ankra za maji ili uweze kuwasaidia," alisema Wilfred.

Alisema wakati anapita mitaani, alishuhudia maji yakimwagika kwenye visima na matangi ya mamlaka za maji, huku umeme mwingi ukitumika.

Mbunifu huyo, alisema mfumo huo utasaidia kupandisha maji kwenye visima na tangi, yakijaa mashine hiyo inajizima.

Alisema kutengeneza mfumo huo kwa mtu binafsi au taasisi ni kati ya Sh. 250,000 hadi Sh. 300,000 kutegemea aina ya pampu itakayofungwa.

Mbunifu mwingine, Obadia John kutoka Klasta ya Karatu, anayesoma Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), alisema alibuni na kutengeneza fimbo nyeupe ya kuhisi kuwasaidia watu wenye ulemavu kutembea barabarani bila vikwazo.

John, alisema vifaa vinavyotumika vinagharimu Sh. 40,000 na matengenezo ya fimbo nyeupe ni Sh. 60,000.

Akizungumzia mpango huo wa kuibua vipaji, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Compassion International- Tanzania, Curthbet Mono, alisema zaidi ya walengwa 65,000 nchini wamehitimu kozi mbalimbali, wakiwemo madaktari, walimu, askari na wauguzi.

Kwa sasa shirika hilo, bado linaendelea kuhudumia watoto 119,000.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo wa Wizara hiyo, Ally Mayai, alipongeza Compassion na makanisa kwa kuwalea vijana na watoto.

Alihimiza maadili kuwa ndio kila kitu kwa wahitimu na vijana nchini.





# Mavunde awaonya wamiliki leseni uchimbaji madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde, amewaonya wamiliki wa leseni za uchimbaji madini nchini kuacha kuichonganisha serikali kwa kuingia mikataba kinyemela na wachimbaji wadogo na wawekezaji wenye mitaji mikubwa. Mavunde alitoa onyo hilo wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa mgodi wa Ntambalale namba mbili uliopo Kijiji cha Wisolele Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga kuhusu mikakati ya serikali kuhakikisha kila mmoja ananufaika na rasilimali hiyo.

Alifafanua kuwa ametoa onyo hilo baada ya serikali kubaini kuwa baadhi ya wamiliki hao wa leseni wamekuwa chanzo kikubwa cha kuichonganisha na wachimbaji wadogo kwa kuwaingiza kwenye maeneo yao na kuanzisha uchimbaji kwa kupeana mirabaha.

Alisema wamiliki hao baada ya kupata wawekezaji wenye mitaji mikubwa, wanakimbilia kwa wakuu wa wilaya kuomba msaada wa askari wa Jeshi la Polisi kuwaondoa wachimbaji hao wadogo kwa nguvu.

Waziri huyo alisisitiza kuwa watakaobainika kuwaweka wachimbaji kwenye maeneo yao kinyemela, serikali itawanyang'anya leseni na kuwapatia wachimbaji waliojiunga kwenye vikundi.

Alisema sheria inamtaka mmiliki kuchimba madini mwenyewe na sio kuingia ubia kinyemela na wachimbaji, kisha kuwaondoa kwa nguvu wanapopata wawekezaji hao, wenye mitaji mikubwa.

"Yeyote mwenye leseni asiingize wachimbaji kwenye leseni yake na kuanza kuchimba madini, jukumu la kulinda leseni isivamiwe ni la mwenye leseni mwenyewe, kama utaingia ubia na wachimbaji hakikisha unafunga mkataba wa kisheria kuondoa migogoro hapo baadaye," alisema Mavunde.

Kwa mujibu wa Mavunde, bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha wa 2024/25 imeongezeka kutoka Sh. bilioni 89 mpaka Sh. bilioni 231 kwa ajili ya kuziwezesha taasisi ya utafiti wa madini na miamba, kununua helikopta ya kufanya utafiti wa maeneo yenye madini na kuwapatia wachimbaji ili kuondoa dhana ya kubahatisha.

Mchimbaji wa mgodi huo, Adrian Lugola, alisema wamekuwa wakiibua maeneo yenye madini na wanapoungana na kikundi kuomba leseni wanaambiwa ni eneo la mtu.

Aliiomba serikali kuyafuta maeneo ambayo hayajaendelezwa na kupewa wachimbaji ili wajikwamua kiuchumi.

Bangili Mkongwe, alisema ili kuondoa matumizi ya kemikali ya Zebaki, ambayo yamekuwa yakihatarisha usalama wa maisha yao kwa kukamata madini bila kuchukua tahadhari, serikali ifunge mashine ya kusaga mawe yenye dhahabu na uchenjuaji wilayani Kahama.

Alisema mashine kama hizo ambazo zimefungwa Katoro mkoani Geita na Itumbi Wilaya ya Chunya Mbeya zimepunguza majanga ya kemikali.

Alisema hivi karibuni Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) waliwatembelea na kuwapatia elimu dhidi ya athari ya zebaki.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Joseph Kumburu, alisema mashine hiyo itafungwa na Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM) hivi karibuni.

Kumburu, alisema wako katika hatua ya usanifu na kwamba eneo la kuweka mashine hiyo imepatikana.



Mchimbaji mdogo kwenye mgodi wa Ntambalale namba mbili, Adrian Lugola, akitoa ombi kwa Waziri wa Madini, Antony Mavunde (hayupo pichani), ya kupewa kipaumbele kurudishiwa leseni iliyofutwa ili kuondokana na kutangatanga kuchimba madini kwa kutumia leseni za watu wengine katika mkutano uliofanyika Kijiji cha Wisolele, Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Watumishi kikaangoni hoja za CAG

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKUU wa Mkoa wa Mara, Evance Mtambi, amelitaka Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Tarime Mjini kuwachukulia hatua baadhi ya watumishi watakaobainika kusababisha hoja za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mtambi alitoa rai hiyo kwenye kikao maalumu cha baraza hilo kilichoitishwa kujibu hoja za CAG kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 unaotarajia kumalizikia hivi karibuni.

"Niliombe baraza hili kuwachukulia hatua za kisheria wale wote ambao walisababisha hoja za ukaguzi, hatua za kuimarisha mifumo ya madeni zichukuliwe haraka, maelekezo ya hoja zote zinazoibuliwa zijibiwe kwa wakati," alisema.

Vilevile alitaka mfumo wa huduma ya ukusanyaji mapato ya kielektroniki (GoTHOMIS) uboreshwe, madiwani na watendaji wapatiwe mafunzo ya umma ya ukusanyaji mapato, mikopo kwa wanawake vijana na watu wenye ulemavu itolewe kwa wakati.

Mweka Hazina wa halmashauri hiyo, George Adino, alisema hoja 19 kati ya 64 zimefungwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alisema kwa ushirikiano walionao watumishi na madiwani wamefanikiwa kupata hati safi kwa miaka minne mfululizo.

Katibu Tawala Msaidizi Usimamizi Ufuatiliaji na Ukaguzi Mkoa wa Mara, Maduhu Malando, alisema serikali imeziba pengo la dawa kutoka Bohari ya Dawa (MSD) baada ya kuja na mfumo ambao umeiwezesha halmashauri kununua dawa kila kunapotokea mahitaji.

Diwani wa Kata ya Turwa, Chacha Machugu, alilipongeza baraza hilo kwa ushirikiano wake na watumishi wa kutekeleza miradi ya kijamii na kupata hati safi kwa miaka minne mfululizo.

# Makandarasi wazembe kuvunjiwa mikataba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, imetishia kuvunja mikataba na makandarasi kwa kushindwa kukamilisha miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa wakati na kuwatia mbaroni.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025 kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Shinyanga Mjini.

Mtatiro, alisema Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), walipokea kiasi cha Sh. milioni 853 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara na kwamba kati ya miradi 10, minne imekamilika.

"Miradi sita ipo ndani ya uwezo wangu, makandarasi wajipange wapo ambao tutavunja mikataba, kuwakamata na kuzuia wasifanye kazi tena hapa Shinyanga," alisema Mtatiro.

Alisema hawawezi kuendelea kufanya kazi na makandarasi wazembe ambao wamekuwa wakikwamisha kukamilika miradi kwa wakati na kudhorotesha shughuli za uchumi zitokanazo na matumizi ya barabara.

Akizungumzia kuhusu huduma za afya, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya Sh. bilioni 1 kukarabati majengo ya Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga.

"Katika utekelezaji wa ilani kwa kipindi hicho, Manispaa ya Shinyanga Rais Samia ametoa kiasi cha Sh. bilioni 35.6, ambazo zimetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu, afya, maji, kilimo, umeme na miundombinu ya barabara," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Shinyanga Mjini, Anorld Makombe, alimpongeza Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa chama hicho taifa kwa kuitekeleza ilani yao kwa asilimia 100 na kufanya mambo makubwa ya maendeleo, ikiwamo ya kimkakati.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Odilia Batimayo, alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia na wasaidizi wake kwa kazi kubwa wanayofanya na watumishi wa serikali kwa kusimamia miradi ya maendeleo.

Nipashe

# Spotika



NYOTA 8 WA COPA AMERICA WA KUANGALIWA NA KLABU 6 ZA EPL UK. 12-13



Cole Palmer (kushoto), akiwa kwenye benchi na wachezaji wenzake wakati England ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na Denmark kwenye michuano ya Euro 2024 nchini Ujerumani Alhamisi iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

# WAKALI WA3 WALIONYIMWA NAFASI ENGLAND EURO 2024

**BERLIN,** Ujerumani

TIMU ya England inahitaji kuimarishwa ili kufurahia mbio nyingi zinazotarajiwa kwenye Euro 2024.

Simba watatu hao wamefuzu kwa hatua ya mtoano baada ya kujikusanyia pointi nne zisizoridhisha katika michezo yao miwili ya mwanzo. Ushindi dhidi ya Slovenia kesho Jumanne utawafanya wawe kileleni mwa kundi na kukabiliana na mpinzani aliye nafasi ya tatu katika hatua ya 16-bora.

Kwenye karatasi, mambo hayaonekani kuwa mabaya sana kwa England. Hata hivyo, haihitaji hasa uchunguzi wa kitaalamu au tathmini ya idadi ya msingi ili kubaini kuwa mambo si mazuri katika kambi ya Kocha Gareth Southgate.

Kocha huyo anatatizika kuweka usawa na England wametoa maonesho mawili ya kustaajabisha kama matokeo. Serbia hawakuwa wa kutosha kuwaadhibu siku ya kwanza ya mechi, lakini Denmark, kwa hisani ya Morten Hjulmand walifanya hivyo.

England imekuwa na mafanikio huku ikitamba sana kwenye michuano iliyopita chini ya Southgate.

Kwa bahati nzuri, Southgate ana chaguzi ambazo bado hajaweza kuzitumia kuwasha kampeni za England. Hawa hapa ni wachezaji watatu ambao hawajacheza hata dakika moja kwenye Euro 2024.

### 1. Cole Palmer

Ni Erling Haaland pekee aliyefunga mabao mengi zaidi ya Ligi Kuu England kuliko Palmer msimu uliopita. Nyota huyo wa zamani wa Man City aliibeba Chelsea mgongoni mwake, na kuandikisha mchango wa mabao 33 kwenye Ligi Kuu.

Kiwango chake cha ajabu kilimfanya aitwe kwenye kikosi cha wachezaji 26 cha Southgate kwa ajili ya michuano hiyo, lakini bosi huyo bado hajamuunga mkono mchezaji huyo.

Palmer ndiye mchezaji wa mwisho 'hufanya mambo kutokea'. Ingawa si mtawala au kiungo katika ukungu wa Jude Bellingham.

Mchezaji huyo wa Chelsea hatarajiwi kuanza mbele ya Bellingham kama namba 10 wa England au zaidi ya Bukayo Saka chini kulia. Hata hivyo, inashangaza kwamba Southgate hajamgeukia Palmer nje ya benchi.

Iwe ni kuisaidia England kuinuka uwanjani katika mabadiliko au kutoa chanzo cha kutoogopa kumiliki mpira, Palmer ana mengi ya kuipatia timu hii. Bila kutaja ustadi wake wa kutoa katika nafasi ya tatu ya mwisho.

### 2. Adam Wharton

Huenda usiwe na kiungo mwenye nywele nyingi zinazotoka labda kipindi kibaya zaidi cha mkopo katika historia ya Ligi Kuu, lakini una Adam Wharton.

Kuinuka kwa kiungo huyo wa Crystal Palace kumekuwa hali ya anga tangu msimu wa baridi alipohamia Selhurst Park, na hakujumuishwa kwenye kikosi cha Southgate kama mchezaji anayecheza soka la kulipwa. Wharton angeweza kuisaidia timu hii ya England inayohangaika.

England wanateseka bila Phillips wa 2021, na mabadiliko ya jumla yanahitajika kutokea ikiwa watafanikiwa kwenye Euro 2024. Wanahitaji kuwa wakali zaidi na Wharton anaweza kuwa hana uzoefu, lakini anaweza kupinga shinikizo na kuvunja mistari.

### 3. Anthony Gordon

Ingawa Palmer ana uwezo wa kuwa mtengeneza tofauti nje ya benchi na Wharton anaweza kukomesha ujanja wa kiungo wa Trent Alexander-Arnold, Gordon anaweza kuwapa England usawa wa kusonga mbele ambao wanakosa sana.

Uhusiano wa Phil Foden na Kieran Trippier haupo chini kushoto, na uchezaji wa England umekuwa wa kutabirika sana kama matokeo. Kwa sasa wanatumia asilimia 70 tu ya uwanja.

Gordon si tu winga wa asili wa kushoto ambaye ni wachezaji wenzake na Trippier kwenye Tyneside, lakini yeye ni mkimbiaji! Kweli anakimbia nyuma!

England si tu inaweka umiliki wao kutoka upande wa kushoto, lakini yote yanatokea mbele ya safu ya nyuma ya mpinzani. Ulinzi huwa mara chache sana, hivyo basi kupunguza nafasi kwa Harry Kane, Foden na Bellingham kucheza.

## ISIKUPITE

KOCHA Hansi Flick ametaja wachezaji sita ambao watazungukwa na nyota wengine kuisuka upya Barcelona, miongoni mwao ni Marc-Andre ter Stegen, Pau Cubarsi, Gavi, Pedri, Fermin Lopez na Lamine Yamal.



# NYOTA 8 WA COPA AMERICA WA KUANGALIWA NA KLABU 6 ZA EPL



DARIO OSORIO

**ATLANTA,**
Marekani

ISITOSHE furaha ya Euro 2024, Copa America 2024 inaendelea huku wachezaji kutoka kote Amerika Kaskazini na Kusini wakipigania utukufu huo wa bara.

**Hata hivyo, miamba ya Ligi Kuu England (EPL), tayari iko bize kutafuta nyota wao wapya huku maskauti wakitumwa kufuatilia kwa karibu nyota kadhaa wa Copa America.**

Hawa hapa ni wachezaji nane ambao klabu sita kubwa za England - Arsenal, Chelsea, Liverpool, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur - wanapaswa kuwaangalia.

**1. Jhon Duran**
**Nchi: Colombia**
**Nafasi: Mshambuliaji**

Chelsea wako mbele kidogo ya mchezo hapa, wakifungua mazungumzo juu ya mshambuliaji huyu wa Aston Villa, Jhon Duran kabla ya mashindano kuanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alilazimika kutulia kwa dakika chache msimu uliopita chini ya Unai, Emery lakini ana matumaini ya kuvutia macho msimu huu wa majira ya joto.

Villa iko tayari kumuuza na inaweza kupokea ofa nyingi kwa Duran.

**2. Valentin Carboni**
**Nchi: Argentina**
**Nafasi: Kiungo mshambuliaji**

Kikosi cha Argentina kimejaa majina ya nyota kama Alejandro Garnacho na Lionel Messi, lakini kuna Valentin Carboni mwenye umri wa miaka 19.

Licha ya kuwa amebakiza miaka minne kwenye mkataba wake na Inter Milan, kuna uvumi mkubwa kwamba kiungo huyo mshambuliaji anaweza kuhama msimu huu wa majira ya joto, huku msimu wa mkopo wa kuvutia huku Monza ukizua uvumi mwingi.

Messi mwenyewe amemuunga mkono hadharani Carboni kuwa sehemu ya mustakabali wa Argentina, ambayo inapaswa kukuambia kila kitu unachohitaji kujua.

**3. Dario Osorio**
**Nchi: Chile**
**Nafasi: Winga**

Winga mrefu, Dario Osorio kwa muda mrefu ametangazwa kuwa mmoja wa vijana wenye vipaji vya hali ya juu Amerika Kusini. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alichukua njia ya kipekee ya kubadilishana Chile na kwenda Denmark aliposajiliwa na Midtjylland, ambao wamefaidika na kipaji chake kwa muda wa miezi 12 iliyopita.

Sio tu kwamba Osorio ameonesha jicho la kweli kwenye bao, lakini amewavutia maskauti. Ikizingatiwa alikabiliwa na maswali juu ya mtazamo wake mapema katika taaluma yake, inaonekana kwamba kijana huyo amefungua ukurasa wa Ulaya.

Takwimu za Osorio zinavutia macho na kuonesha kuvutia msimu huu wa majira ya joto kunaweza kufungua mlango wa harakati nyingine kubwa nje ya nchi.

**4. Malik Tillman**
**Nchi: Marekani**
**Nafasi: Kiungo mshambuliaji**

Msimu wa 2023/24 ulikuwa mwaka wa mapumziko kwa Malik Tillman, ambaye aliondoka Bayern Munich kwa mkopo na kwenda PSV Eindhoven.

Akiwa na mabao tisa na asisti 11 katika mechi 28 pekee, Tillman alionesha uwezo wa kufanya matokeo ya kweli katika safu ya juu, na kiungo huyo mrefu sasa anarejea Munich akijiuliza nini kitafuata kwa mustakabali wake anapoingia miaka miwili ya mwisho ya mkataba wake.

Akiwa amestarehe kati na winga ya kushoto, Tillman ana shinikizo nyingi mabegani mwake kwenye Copa America, hivyo maskauti wanaweza kupata mwanga wa nguvu zake za kiakili kuendana na ubora wake wa kiufundi.

**5. Willian Pacho**
**Nchi: Ecuador**
**Nafasi: Beki wa kati**

Willian Pacho ni beki wa kati mwenye umri wa miaka 22, anayetumia mguu wa kushoto. Hiyo ni kama vumbi la dhahabu katika soko la leo.

Liverpool tayari wanahusishwa na kutaka kumnunua Pacho msimu huu wa majira ya joto baada ya kiwango chake cha kuvutia akiwa na Eintracht Frankfurt kwenye Bundesliga. Ana raha kwenye mpira na anafurahi kuanzisha mambo kutoka nyuma, lakini pia anaweza kutupa sura yake yenye nguvu ili kuwalemea washambuliaji.

Pacho ana miaka minne kwenye mkataba wake, lakini Frankfurt haitaweza kupinga ofa kubwa.

**6. Guido Rodriguez**
**Nchi: Argentina**
**Nafasi: Kiungo mkabaji**

Guido Rodriguez anaondoka Real Betis msimu huu wa majira ya joto na anapatikana kwa uhamisho wa bure, ambao tayari unapaswa kuvutia mazingira ya Ligi Kuu.

Akiwa na umri wa miaka 30, Rodriguez si usajili wa muda mrefu kwa mtu yeyote, lakini anakuja na uzoefu wa miaka kadhaa akiimarisha moja ya safu ya kiungo kali kwenye La Liga.

Ripoti zinaonesha Barcelona wako mbioni kuzima moto, lakini timu hiyo ya Katalunya haiwezi kushindana na mishahara inayotolewa nchini Uingereza.

**7. Joel Ordonez**
**Nchi: Ecuador**
**Nafasi: Beki wa kati**

Ecuador ni moja ya sehemu ya kusafirisha nyota wa siku zijazo, lakini safu hiyo ya uzalishaji imesonga kwa kasi na kwa ukali sana katika miaka ya hivi karibuni, kwani beki wa kati Joel Ordonez ameruka chini ya rada.

Akiwa bidhaa ya akademi ya Independiente del Valle, Ordonez mwenye umri wa miaka 20 alijiunga na Club Brugge mwaka wa 2022 na akajiweka kivyake mwishoni mwa msimu uliopita, na kuisaidia timu yake kutwaa taji lingine la ligi.

Ordonez ni jasiri katika safu ya ulinzi na anaonyesha uwezo mkubwa kama mchezaji kutoka nyuma, na klabu kubwa zitakuwa zimejaa kuwania saini yake.

**8. Santiago Gimenez**
**Nchi: Mexico**
**Nafasi: Mshambuliaji**

Santiago Gimenez wa Feyenoord ni mwingine ambaye sifa yake tayari imedai kutembelewa na mawakala wa Ulaya. Alifunga mabao 23 kwa Feyenoord ya Arne Slot msimu uliopita, baada ya kumaliza kampeni ya awali kwa kufunga mabao 12 katika mechi 16.

Akiwa na umri wa miaka 23, Gimenez bado yuko kazini, lakini ana uwezo mkubwa wa kukuza na kuwa mshambuliaji nyota, na ingawa idadi kubwa ya Eredivisie haijachangia mafanikio ya Ligi Kuu kila wakati, hakuna sababu ya kuamini kwamba nyota huyo wa Mexico hataweza kufunga mabao akiwa EPL.

Jambo kuu sasa, hata hivyo, ni jinsi Gimenez anavyokabiliana na mfumo tofauti na ule wa kocha mpya wa Liverpool.

## Nukuu



"Ni muhimu kutambua nini mchezaji anachokupa. Cristiano anakupa uzoefu, anakupa fursa ya goli, mbali na kufungua nafasi. Cristiano ni mchezaji wa timu ya taifa na anastahili kuwa hapa, ninachotazama tu ni nini alichofanya na kipi amekifanya katika mashindano yaliyopita. Ni mchezaji mwenye nidhamu sana, mpiganaji na ni muuaji, mchezaji muhimu sana kwenye boksi," **Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Ureno, Roberto Martinez, akizungumzia umuhimu wa Cristiano Ronaldo kwenye michuano ya Euro 2024 nchini Ujerumani.**



"Sidhani Tedesco ni mkufunzi mzuri wa Ubelgiji. Ingawa hana ukaidi wa Roberto Martineza. Leandro anakosolewa, lakini alihamishwa kutoka nafasi moja hadi nyingine. Kwa njia hiyo huwezi kupata mstari katika mchezo wako. Usiwadharau Waromania hao, Ukraine haikuhusika katika mechi yao ya kwanza. Lakini natumai nimekosea, Wabelgiji wanashinda na shauku inapamba moto," **Baba mzazi wa Leandro Trossard, akimtaja Kocha wa Ubelgiji, Domenico Tedesco, kuwa anapaswa kulaumiwa kwa kiwango kisichoridhisha cha mwanawe kwenye mchezo wa ufunguzi wa Euro 2024 dhidi ya Slovakia.**




"Msimamo wa klabu yangu ulikuwa wazi sana, kwa hivyo kuanzia wakati huo, nadhani nilijua sitashiriki. Hivyo ndivyo ilivyo, na ninaelewa hilo pia. Ninajiunga na timu mpya Septemba, kwa hivyo si njia bora ya kuanza safari," **Kylian Mbappe akithibitisha kuwa hatakuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kitakachoshiriki mashindano ya Olimpiki baadaye mwaka huu nchini humo.**

# WACHEZAJI 11 WANAOTAJWA KUTUA SIMBA MSIMU UJAO


JOSHUA MUTALE

**Na Adam Fungamwango**

TANGU dirisha kubwa la uhamisho wa wachezaji kufunguliwa Juni 15, mwaka huu, Klabu ya Simba ndiyo imeongoza kuwa na tetesi nyingi za usajili kuliko zingine zote hapa nchini.

**Inawezekana ni kwa sababu ya mahitaji, kwani hata viongozi wake kwa nyakati tofauti wamesema wanataka kufanya usajili mkubwa kwa kuondoka wachezaji wengi, ambao baadhi umri umekwenda, wengine wamelewa mafanikio, na wapo wanaotajwa kuwa na nidhamu isiyoridhisha na walioshuka viwango pia.**

Kutokana na hilo, inawezekana kabisa msimu ujao, Simba ikawa moja kati ya timu zitakazosajili wachezaji wengi ili kuunda kikosi kipya chenye uchu wa mafanikio.

Katika makala haya tunakuletea tetesi za wachezaji 11 ambao wanatajwa kuwa huenda wakavaa uzi mwekundu na timu zao walizotoka, ukimwondoa Lameck Lawi kutoka Coastal Union ambaye klabu imeshathibitisha.

### 1# Omari Omari- Mashujaa FC

Hadi kufikia jana, klabu hiyo ilikuwa katika hatua za mwisho kumsajili straika Omari Omari kutoka Mashujaa FC. Habari zinasema kuwa kuna vitu vichache tu vimebaki kabla ya nyota huyo wa zamani wa Prisons kutambulishwa katika dirisha hili kubwa la usajili.

### 2# Rahim Shomari- KMC

Taarifa zinaeleza kuwa Simba inapigana huku na huko kuhakikisha inapata saini ya beki wa kushoto wa KMC, Rahim Shomari, ili kusaidiana na Mohamed Hussein 'Tshabalala.'

Chanzo hicho kimesema kuwa KMC ambayo makuzi yake yalianzia kwenye kikosi cha vijana cha Simba, anatajwa kwenda Msimbazi, huku klabu yake ikihitaji kiasi cha Sh. milioni 100 ili kumwachia.

### 3# Anthony Tra Bi Tra- Asec Mimosas

Inatajwa pia kuwa Simba iko kwenye mazungumzo na beki wa kati wa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Anthony Tra Bi Tra ili kuziba pengo la beki Henock Inonga ambaye kwa siku za karibuni amepoteza mapenzi kwa wanachama na mashabiki wa Simba.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema baada ya kupata saini ya Lameck Lawi, sasa wanasaka beki mmoja kutoka nje ya nchi ambaye atakuja kusaidiana na waliopo.

### 4# Derrick Fordjour- Medeama

Katika kusaka mastraika watakaoiwezesha timu kurudi kwenye makali yake, imeelezwa kuwa ipo mbioni kukamilisha dili la kumsajili straika wa Medeama ya Ghana, Derrick Fordjour. Watanzania walimshuhudia msimu uliopita, akiwa kwenye kiwango cha juu, katika Ligi ya Mabingwa Afrika, timu yake ikiwa kundi moja na Yanga.

### 5# Pedro Miguel- Petro de Luanda

Katika kuhangaikia kusaka kiungo mkabaji, taarifa zinaeleza klabu hiyo imetua nchini Angola kusaka saini ya Pedro Miguel wa Petro de Luanda ambaye alikichafua msimu uliopita katika klabu yake hiyo na kuifanya kuongoza Kundi C, kabla ya kutolewa na TP Mazembe katika hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

### 6# Ricky Banda- Red Arrows

Taarifa zinasema Simba imeanzisha mazungumzo na straika Ricky Banda anayekipiga katika Klabu ya Red Arrows ya Zambia.

Straika huyo amemaliza Ligi Kuu ya Zambia akiwa na mabao 10 na kuwa kinara wa ufungaji, akifungana na wachezaji wengine wawili waliofunga idadi kama hiyo ya mabao, Enock Sakala wa Zesco United na Prince Mumba wa Kabwe Warriors.

### 7# Agostinho Mabululu- Al Ittihad

Alitamba sana kwenye fainali za AFCON zilizofanyika mapema mwaka huu nchini Ivory Coast akiwa na timu yake ya Taifa ya Angola. Straika huyu anayeichezea Al Ittihad ya Misri naye anatajwa kuwa mmoja wa wachezaji ambao Simba wanachangamka ili atue Msimbazi.

### 8# Jean-Marc Makusu- Hajer FC

Mwanzoni kabisa wakati dirisha la usajili linafunguliwa, zilikuja taarifa zinazohusu klabu hiyo kuwa na mazungumza na straika wa zamani wa AS Vita, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean-Marc Makusu Mundele ili kusaidia eneo la ushambuliaji.

Kwa sasa anaichezea Klabu ya Hejer FC ya Saudi Arabia na amekuwa akihusishwa na Simba kwa misimu kadhaa ya hivi karibuni.

### 9# Augustine Okejepha- Rivers United

Taarifa hizi zimetoka juzi kuwa Simba iko mbioni kukamilisha dili ya kusajili kiungo mkabaji, Augustine Okejepha kwa mkataba wa miaka mitatu.

Mchezaji huyo aliyeonyesha kiwango kikubwa katika mechi za Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita akiwa na River United ya Nigeria, ameonyesha kukubaliana kila kitu na klabu hiyo na sasa kinachosubiriwa ni utekelezaji.

### 10# Kelvin Kapumbu- Zesco United

Simba pia inadaiwa kuwa na mazungumzo na kiungo huyu wa Zesco ya Zambia, kuja kuimarisha eneo hilo ambalo limeonekana kwa miaka ya hivi karibuni linasuasua kitu ambacho si utamaduni wa klabu hiyo.

### 11# Joshua Mutale- Power Dynamos

Inaelezwa kuwa winga huyu machachari wameshasainiana mkataba wa miaka mitatu kuitumikia klabu hiyo kutoka Power Dyanamos ya Zambia, kinachosubiriwa ni utambulisho tu.

Winga huyo aliyemaliza ligi na mabao manane, anakumbukwa na mashabiki wa Simba, kwani aliwachachafya mabeki wa timu hiyo, hasa Shomari Kapombe katika mechi tatu ambazo timu hizo zimekutana, moja ya Simba Day na zilizobaki ni za Ligi ya Mabingwa Afrika katika hatua za awali msimu uliopita.

**JE, WAJUA?**



TIMU ya Boston Celtics ndiyo inayoshikilia rekodi ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mpira wa Kikapu nchini Marekani baada ya msimu huu wa 2023/2024 kuubeba kwa mara ya 18, ikifuatiwa na Los Angeles Lakers iliyobeba mara 17.



# TBA, sekta binafsi kushirikiana ujenzi wa nyumba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Huduma Saidizi kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Mathias Mhembe, amesema wataendelea kushirikiana na sekta binafsi kufikia malengo yaliyowekwa na serikali, ikiwamo ujenzi wa nyumba za watumishi 10,000.

Amesema nyumba hizo ni kwa ajili ya watumishi wa serikali ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020.

Mhembe alisema hayo jana jijini hapa baada ya kutembelea banda la maonesho ya wakala huo kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika viwanja vya Chinangali.

Alisema TBA inawajibu wa kutekeleza mambo matatu ikiwamo kujenga nyumba za serikali, ushauri wa majengo ya miradi mbalimbali inayojengwa pamoja na kusimamia miliki za serikali.

Alisema katika kutekeleza maagizo ya serikali wakala huo utaendelea kushirikiana na sekta binafsi kukamilisha malengo mbalimbali yaliyowekwa na serikali.

"Wakala wa Majengo Tanzania unayo majukumu matatu ya kuteleza ikiwamo kujenga nyumba za serikali, kutoa ushauri wa ujenzi wa miradi ya majengo mbalimbali yanayojengwa lakini kusimamia miliki za serikali," alisema.

Aidha, alisema lengo la kushiriki maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ni kutoa huduma za moja kwa moja kwa wananchi ili wapate mrejesho kwa ajili ya kufanyia kazi. "Tupo hapa kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali lakini kupata mrejesho wa huduma zetu ambazo tunatoa kwa wananchi ili tuweze kufanyia kazi yale mapungufu ambayo tutaelezwa," alisema.

Kadhalika, alisema TBA wanaendelea kutumia mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) iliyoandaliwa na serikali kutoa huduma kwa wateja.

"Lakini pia tunatumia mifumo hiyo kwa ajili ya watumishi wetu ukiwamo ule wa kupima utendaji kazi wa watumishi wetu ili kutoa huduma bora kama mkataba wa huduma kwa wateja unavyotutaka," alisema.

Alisema mkataba wa huduma kwa wateja unawataka kutoa huduma bora kwa wateja wa ndani na nje.

Alisema: "Hivyo basi nitowe wito kwa Watanzania na wageni kutoa nje kuja kupata huduma bora zinazozingatia takwa la mkataba wa huduma kwa wateja".



Mwanafunzi wa Chuo cha Donbosco Technical Institute of Dodoma Klasta ya Kiteto, Abednego Wilfred (aliyeinama), ambaye amebuni mfumo wa 'Automatic Pump' wa namna ya kudhibiti upotevu wa maji akimwonesha Mkurugenzi wa Michezo kutoka Wizara ya Utamaduni na Michezo, Ally Mayai Tembele (nyuma yake) na viongozi wa Shirika la Compassion International Tanzania ambao ndio wafadhili wake pamoja makanisa ya kipentekoste kwenye tamasha la kuibua vipaji Kanda ya Ngorongoro, lililofanyika katika Shule ya Sekondari Singe wilayani Babati mkoani Manyara mwishoni mwa wiki. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Watanzania wahimizwa kuomba pasipoti kwa wakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, amewasihi Watanzania kujenga utaratibu wa kuomba pasipoti kwa wakati na kuepuka kusubiri hadi wanapopata safari.

Alitoa rai hiyo juzi jijini hapa, alipotembelea maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika viwanja vya Chinangali Park.

"Kutokana na mfumo maalumu wa kielektroniki sasa hivi mwananchi anaweza kupata pasipoti kwa muda mfupi kupitia njia ya mtandao, tusisubiri safari ndipo ukaombe.

Hii ni haki yako hivyo serikali imeturahisishia huduma tupo kila mahali kuwahudumia," alisema.

Aidha, alitoa hamasa kwa wananchi kuyatumia maonesho hayo kupata huduma za vitambulisho vya taifa ili kuepusha usumbufu wanapohitaji huduma mbalimbali za kijamii "Kati ya wananchi wa Tanzania milioni 61, milioni 32 wamekadiriwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwamba wamefikia umri wa kuweza kusajiliwa, kati ya hao tayari vitambulisho milioni 24 vimeshatengenezwa na vitambulisho zaidi ya milioni 19 vimetolewa," alisema.

Katika ziara hiyo, Katibu Mkuu Gugu alipokelewa na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Miriam Mmbaga na kutembelea mabanda yote ya wizara pamoja na vyombo vyake vya usalama.

Vile vile, alitumia fursa hiyo kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kujipanga madhubuti katika kutoa elimu na kuhudumia wananchi wanaotembelea mabanda ya wizara hiyo.

# NGOs zakumbushwa kufuata mila, desturi za kitanzania

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema mashirika yote yasiyo ya kiserikali nchini yanapaswa kufanya shughuli zao kwa kwa mujibu wa malengo waliyosajiliwa na kujiepusha na vitu ambavyo ni kinyume na mila na desturi za kitanzania.

Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mussa Sang'anya alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO).

Sang'anya alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya usajili wao ili kujiepusha na vitu ambavyo vinaweza kuvunja mila na desturi za kitanzania.

"Mashirika yote yasiyo ya kiserikali nchini yanapaswa kuzingatia malengo ya usajili wao ili kutekeleza yale yanayoendana na usajili kinyume na hapo serikali itachukua hatua," alisema.

Kuhusu mafunzo alisema wajumbe hao watapitishwa katika mambo mbalimbali ikiwamo Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kanuni na taratibu za uendeshaji mashirika.

"Mafunzo haya ni semina elekezo kwa wajumbe wa baraza ili kuwajengea uwezo wa kupata uelewa namna ya kuendesha mashirika yao kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Lakini pia watafundishwa namna ya kusimamia mashirika mengine nchini na kufanya kazi na yale yanayotoka nje ya nchi bila kuvunja sheria pamoja na mila na desturi zetu" alisema.

Kadhalika, alisema kutoka na dhamana yaliyonayo mashirika hayo ya kupeleka maendeleo kwa wananchi na kuwaunganisha na serikali mafunzo hayo yatakuwa tiba kwa changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza.

Alisema: "Tunayo mashirika takribani 9,000 nchini hivyo chombo hiki ni muhimu sana kwa taifa. Mafunzo haya yatasaidia kuwajengea uelewa wa kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia sheria na mila na desturi zetu".

Mwenyekiti kamati ya mpito ya kuratibu uchaguzi mashirika yasiyo ya kiserikali, Christina Ruhinda alisema wajumbe 30 wa NaCoNGO ndiyo watapatiwa mafunzo hayo.

Alisema baada ya uchaguzi ulioanzia ngazi ya wilaya na badaye mkoa, kwamba walipatikana wajumbe 26 ambao wameungana na wawakilishi wa vijana, wenye ulemavu, watoto pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa.

Mratibu wa mafunzo hayo, Ntimi Charles, alisema lengo ni kuwajengea uwezo wajumbe wa baraza hilo ili kuwa na uelewa wa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Alisema pamoja na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi pia wanawafundisha namna ya kufanya kazi na mashirika kutoka nje ambayo yanakuja na taratibu zao.





# Mtaka: Madiwani acheni unafiki, porojo

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe wametakiwa kuacha fitina na porojo kwa ajili ya kuleta maendeleo katika kata zao na kwa wananchi.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati akizungumza kwenye Baraza la Madiwani la halmashauri hiyo kujadili hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mwishoni mwa wiki iliyopita.

Mtaka, alisema madiwani wanapaswa kuepuka unafiki na porojo kuelekea mwaka huu wa mwisho kabla ya kufanyika Uchaguzi Mkuu ujao wa 2025 wa wabunge na madiwani.

"Porojo, majungu, fitina sio sehemu ya ajenda ambazo mwakani mtajaza fomu mwezi wa saba (julai), sifa ya fitina huwa haipo, ningetamani kuona watu wanapendana kwa sababu bila ya kufanya hivyo matokeo yake mnaharibu halmashauri yenu," alisema.

Alisema kwenye siasa pigana vita fupi, majeruhi wachache si kupigana vita ndefu ambayo itagharimu muda, nguvu za fedha na za damu.

"Nyie mnapigana vita miaka mitano, jifunzeni kumaliza vitu nyinyi ni wanasiasa, wazazi na walezi. Miaka mitano hapana kwa sababu najua kuna watu humu hamsalimiani," alisema Mtaka.

Alisema kila mmoja anapaswa kuonyesha miradi viporo ili iweze kupewa kipaumbele na kujenga taswira ya kazi zilizofanyika katika kipindi hicho cha miaka mitano kuanzia 2020 mpaka 2025.

"Tuna miradi viporo mingi sana kwenye halmashauri kila mmoja kwenye kata yake, wananchi walichanga wakataka zahanati wakaishia kwenye lenta, wakachimba kamsingi kwenye ofisi ya kijiji kakaishia hapo, wakafanya hivi ikaishia hapa, kwenye mwaka mmoja uliobaki lazima nyinyi wenyewe mkubaliane," alisema Mtaka.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omari, aliwapasha madiwani kuwa fitina siku zote sio jambo jema kwa sababu wote wanatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka mitano.

"Shikaneni na mnapozungumza jambo muende kwa pamoja kwa hiyo mimi nawaomba tuache fitina na masuala ya figisu figisu hapana," alisema Omari.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Peter Nyanja, alisema taarifa ya ukaguzi wa mradi wa Mfuko wa Kukopesha Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu (WYDF) kwa mwaka 2022/2023, halmashauri ilikuwa na hoja nne, kati hizo, mbili sawa na asilimia 50 utekelezaji wake umekamilika na kufungwa.

Nyanja alisema halmashauri hiyo pia ilikuwa na hoja moja ya miaka ya nyuma ambayo imefanyiwa kazi kwa sehemu.



Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kata ya Tandala wilayani Makete, Mkoa wa Njombe, Rehan Abuu, akiwa na familia ya Farijala Tuli ambayo ina mtoto mwenye ualbinona kuwatoa hofu kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kuwalinda watoto wenye ualbino kwa kuwa nao ni sehemu ya jamii na wanapaswa kuishi kama watu wengine. **PICHA: ELIZA KILINDI**

# TBS yateketeza bidhaa za mamilioni

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), Nyanda za Juu Kusini limeteketeza tani 7.2 za bidhaa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 43 baada ya kwisha muda wake wa matumizi na vipodozi vilivyopigwa marufuku kutumika nchini.

Baadhi ya bidhaa hizo zilizoteketezwa ni vinywaji vyenye vilevi vilivyokwisha muda wake wa matumizi bia, mvinyo, juisi, soda na vyenye visisimuzi mwilini.

Nyingine ni mafuta ya kula, biskuti, maziwa ya watoto, nyanya na pilipili za kwenye chupa na siagi na vipodozi venye viambata sumu venye madini yakiwemo ya zebaki, tembo na Hydroquinone.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa wakati wa kuteketeza bidhaa hizo, Meneja wa TBS Nyanda za Juu Kusini, Abel Mwakasonga, alisema bidhaa hizo zilikamatwa kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi Juni mwaka huu kufuatia ukaguzi uliofanyika halmashauri za mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Iringa.

Alitaja miongoni mwa madhara ya kiafya yanayosababishwa na bidhaa hizo kuwa ni magonjwa ya matumbo, saratani.

Kwa upande wa vipodozi hivyo, alisema vinaondoa asili ya ngozi na kusababisha madhara katika mwili wa binadamu.

Alitoa rai kwa wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa bidhaa kuhakikisha kuwa wanaingiza sokoni ambazo zimethibitisha ubora wake na TBS, vinginevyo zitaondolewa sokoni na kuteketezwa kwa gharama zao wenyewe.

Kwa mujibu wa sheria ya viwango ni marufuku kwa wazalishaji, wasambazaji na wauzaji kuingiza kwenye Soko la Tanzania bidhaa ambazo hazijathibitishwa ubora wake na TBS.

Mwakasonga aliwataka wananchi kutotumia bidhaa ambazo hazijathibitishwa na TBS zikiwemo zile zilizopigwa marufuku kutumika nchini vikiwamo vipodozi vyenye viambata sumu.

Alisisitiza wananchi kusoma taarifa zilizopo kwenye vifungashio vya bidhaa wanazotaka kununua ili kujua kama hazijaisha muda wake wa matumizi na kama zimethibitishwa na shirika hilo.

# Shirika latakiwa kukamilisha utafiti mbolea ya mimea

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

SHIRIKA la Maendeleo ya Kilimo Njombe (NADO), limetakiwa kukamilisha utafiti wa mbolea aina ya Biochar inayotengenezwa kwa mabaki ya mimea.

Mbolea hiyo inayotengezwa kwa nyasi, majani, vibunzi vya mahindi na miti ya mbao inatajwa kufanya kazi mbadala wa chokaa mazao kwa kurudisha afya ya udongo ili kuwasadia wakulima kuzalisha kwa tija.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Msaidizi wa Uratibu na Ufuatiliaji wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Grace Mbwilo wakati wa ufuatiliaji wa kazi zinazofanywa na NADO katika Kijiji cha Nyumbanitu kilichopo wilayani hapa.

Mbwilo, alilitaka shirika hilo kukamilisha utafiti huo ili mbolea hiyo itumiwe na wananchi wa maeneo mengine.

Alisema endapo utafiti huo utakamilika na kuleta matokeo chanya utakuwa na faida kwa wakulima kwani watazalisha mbolea hiyo kwa gharama nafuu na kuwasaidia kuleta tija kwani udongo kurejea katika hali yake.

"Wakulima wengi wanalima mahindi, lakini vigunzi wanavitupa sasa tukiweza kupata matokeo mazuri ya kitu kama hiki watu wanaweza kusaga na kuuza inakuwa ni biashara pia na kuboresha uzalishaji wa mazao, watafiti wetu mtusaidie sasa tuone matokeo ya hii mbolea ya samadi ukichanganya na vigunzi," alisema.

Baadhi ya wanachama wa Kikundi cha Umoja cha Nyumbanitu, akiwamo Cosmas Mfugale na Liston Kilumile, waliitaka serikali kushirikiana na shirika hilo kupata mbegu bora za viazi, mahindi na parachichi ili yajumuishwe katika kilimo mseto badala ya kutegemea cha zao moja pekee.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Keneth Msigwa, alisema utafiti huo utawasaidia kuzalisha mazao kwa tija kutokana na udongo kurejeshwa katika hali yake.

"Wananchi wamejifunza kuwa huu utafiti unatusaidia kwa sababu tukiutumia na huko mashamba yetu ya mitaani tutabadilika kiuchumi kwa sababu tuna uhakika tukitumia samadi kwa wingi kwenye udogo wetu huu hali ya uzalishaji ya zamani itarudi," alisema Msigwa.

Ofisa Utawala wa NADO, Ernest Ng'umbi, alisema wameanza kufanyia kazi utafiti huo wa uzalishaji wa chokaa mbadala ya mazao ili kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija baada ya kutegemea kupata msaada kutoka Finland.



## Waziri: Toeni taarifa mkipewa huduma mbovu hospitalini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imewataka wananchi wanaofika katika hospitali za serikali wasisite kutoa taarifa endapo hawataridhishwa na huduma walizopewa ili hatua za kinidhamu zichukuliwe.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, aliyasema hayo wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Nungwi, Abdallah Abasi Wadi aliyehoji kwamba bado yako malalamiko yanayohusiana na manyanyaso wanayoyapata wananchi.

Akijibu swali hilo, Hassan alisema wizara yake imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kiutumishi kwa watumishi wanaoendana kinyume na utaratibu wa kazi.

Alisema lengo kuu la Wizara kupitia watendaji wake ni kutoa huduma bora na stahiki kwa wananchi wote bila ya ubaguzi na katika kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Katika hatua nyingine akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe aliyetaka kujua kwa kiasi gani mfumo unaorahisisha taarifa za mgonjwa kuweza kusomeka na kufahamika katika kila eneo la hospitali husika kwa kiasi gani umeweza kurahisisha upatikanaji wa huduma kulingana na dhamira iliyokusudiwa.

Naibu waziri huyo alisema wizara imeanzisha mfumo unaorahisisha taarifa za mgonjwa kuweza kusomeka na kufahamika katika kila eneo la hospitali husika kutoka mapokezi hadi kwenye eneo la dawa.

Alisema mfumo huo umeanza kwa hatua za majaribio katika baadhi ya hospitali na vituo vya afya ikiwemo Makunduchi, Kitogani, Kivunge, Chakechake, Micheweni, vitongoji, Abdalla Mzee na Rahaleo.

Alisema lengo ni kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzifanyia kazi kabla kuanza kuutumia rasmi katika vituo vyote Unguja na Pemba.

Aidha, alisema wastani wa watendaji 50 kutoka katika kila kituo cha afya na hospitali husika wamepatiwa mafunzo ili kuweza kuendana na lengo lililokusudiwa.

# Idadi ya wageni wanaoingia Zanzibar yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wageni walioingia visiwani Zanzibar katika kipindi cha Mei mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 12.7 kutoka 26,620 mwaka jana hadi 29,995 kipindi kama hicho mwaka huu.

Ofisa Takwimu kutoka Kamisheni ya Utalii, Hassan Ameir Vuai, alitoa taarifa hiyo alipokuwa akiwasilisha takwimu za uingiaji wageni kwa mwezi Mei mwaka huu.

Alisema ukilinganisha na Aprili 2024, idadi hiyo imeonyesha ongezeko la asilimia 3.4 kutoka wageni 28,995 walioingia mwezi huo.

Ameir aliitaja Ujerumani ndiyo iliyoongoza kwa kuleta wageni wengi wapatao 5,261 sawa na asimilia 17.5 ya wageni wote ikifuatiwa na Ufaransa iliyokuwa na wageni 3,009 asilimia 10.3.

Alisema Marekani imeshika nafasi ya tatu kwa kuingiza wageni 2,373 sawa na asilimia 7.9, huku Afrika Kusini ikishika nafasi ya nne kwa kuingiza wageni 1,819 sawa na asilimia 6.1 na ya tano ilikuwa Uingereza iliyokuwa na wageni 1,708 sawa na asilimia 5.7.

Alisema wageni 17,297 waliingia nchini kutoka Ulaya sawa na asilimia 57.7, huku Afrika likifuatia kwa kuwa na wageni 5,928 sawa na asilimia 19.8.

"Bara la Amerika lilikuwa la tatu kwa kuwa na wageni 3,233 sawa na asilimia 10.8 na Antaktiki lilikuwa na wageni 493 sawa na asilimia 1.6," alisema.

Alisema wageni 25,224 sawa na asilimia 84.0 waliingia Zanzibar kupitia katika viwanja vya ndege na wageni 4,771 sawa na asilimia 16.0 waliingia kupitia bandarini.

"Wageni 15,257 asilimia 50.9 walikuwa ni wanaume na wageni 14,738 asilimia 49.1 walikuwa ni wanawake," alisema Vuai.

Aidha, alisema asilimia 94.4 ya wageni walikuja nchini kwa ajili ya mapumziko, huku asilimia 0.6 walikuja kwa lengo la kuwatembelea ndugu na marafiki na asilimia 4.9 waliingia kwa ajili ya sababu nyinginezo lakini asilimia 0.1 ya wageni walikuja kwa ajili ya biashara na mikutano.

Mkurugenzi Rasilimali Watu, Mipango na Utawala Kamisheni ya Utalii, Aviwa Issa Makame, alisema serikali imejipanga kuongeza idadi ya watalii kwa kuendelea kuviimarisha vivutio vya utalii na utoaji wa huduma bora wanapofika nchini.

Ofisa Uhusiano kutoka Jeshi la Uhamiaji Zanzibar, Shariff Bakar Shariff, alisema idara hiyo imeimarisha huduma zake ikiwamo kuimarisha mifumo ya kielektroniki kwa kuwawezesha wananchi na wageni kuomba visa kwa urahisi zaidi.

Alisema huduma hiyo imesaidia kuepusha usumbufu kwa waombaji ndani na nje ya Zanzibar.



Wasaidizi wa sheria kutoka visiwa vya Pemba na Unguja wakipewa mafunzo rejea ya siku mbili kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Haki za Binadamu yaliyoendeshwa na Mwenyekiti wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Profesa Chris Peter Maina, mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Maambukizi VVU kwa vijana, watoto yashika kasi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Watu wanaoishi Virusi Vya Ukimwi Zanzibar (ZAPHA Plus), Hasina Hamad, amesema kuna ongezeko la watoto na vijana wanaoishi na VVU visiwani hapa, ambao wanahitaji msaada wa huduma za msingi.

Aliyasema hayo katika hafla ya utiaji saini mkataba wa ushirikiano katika kupambana na VVU kati ya jumuiya hiyo na Baraza la Watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI Tanzania Bara (NACOPHA).

Mwenyekiti huyo alisema juhudi za pamoja zinahitajika ili kuhakikisha wanaoishi na VVU wanapata matibabu, huduma na matunzo yanayostahiki yatakayoelekea kupunguza na kuondokana na maambukizi mapya ya VVU.

Hasina alisema ushirikiano huo ni moja kati ya hatua ya kufikia malengo yao ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU hasa ikizingatiwa kuwa VVU.

Alisema bado kuna unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU katika jamii hususani sehemu za kazini, shuleni, hospitali.

Hasina alisema hivyo mkataba huo wa ushirikiano utasaidia katika kupambana na janga la UKIMWI na kupunguza unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU.

"Utashangaa hadi katika vituo vya afya kuna unyanyapaa kwa watu anaoishi na VVU na kila sehemu unyanyapaa umetawala ingawa umepungua kidogo tofauti na miaka ya nyuma," alisema.

Aidha, alisema kipindi cha nyuma kulikuwa na changamoto ya ongezeko la kasi ya VVU na wimbi la vifo vitokanavyo na UKIMWI kutokana na kutokuwepo kwa dawa za kupunguza makali pamoja na ongezeko kubwa la watoto yatima.

Alisema pia kulikuwa na changamoto ya ongezeko maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto kutokana kutokuwapo na huduma za kinga.

Alisema hivi sasa kuna juhudi kubwa zinazofanywa na serikali pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya VVU ikiwamo mabadiliko ya kisera na kimkakati katika mapambano hayo na kuimarisha huduma za utoaji wa matibabu na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU.

Hasina alisema mapambano hayo ni pamoja na upatikanaji wa dawa za kupunguza makali na kuimarika kwa huduma za kinga za kuzuwia maambukizo kutoka kwa mama na mtoto.

Hata hivyo, alisema changamoto zinazowakabili kwa sasa ni unyanyapaa, utegemezi mkubwa kutoka kwa wafadhili katika upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya VVU na huduma zingine muhimu kwa sababu dawa hizo ndiyo maisha yao.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya NACOPHA, Leticia Mourice alisema mkataba huo wa ushirikiano utatengeneza umoja wa kufanya kazi kwa pamoja katika mapambano ya VVU na UKIMWI na wana kila sababu ya kuchagua shughuli ya kufanya kwa pamoja ambayo viongozi wa serikali zote mbili kuona umuhimu wa umoja huo.

Mkurugenzi wa Tume ya UKIMWI Zanzibar, Dk. Ahmed Muhammed, alisema utafiti wa viashiria vya UKIMWI na tabia hatarishi umeonesha mafanikio kwa kupunguza maambukizi mapya ya VVU ingawa bado kuna changamoto ambapo mkataba huo wa mashirikiano utaisaidia kutatua changamoto hizo.

# Zaidi wataalamu 400 leo kutibu, kupima wananchi bure

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa afya 450 kutoka hospitali mbalimbali nchini na taasisi 40 wanatarajiwa kutoa matibabu na vipimo bila malipo kwa siku saba kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha.

Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda (pichani), alibainisha hayo mwishoni mwa wiki baada ya kukagua maandalizi ya kliniki hiyo ya afya inayotarajiwa kuzinduliwa leo kwenye Uwanja Sheikh Amri Abeid.

Alisema wataalamu hao, wakiwamo madaktari bingwa watatoa matitabu kwa wananchi bila gharama yoyote, hivyo ni muhimu wakajitokeza kwa wingi na kutibiwa.

"Ninaomba kuwakaribisha wananchi wote wa Arusha kujitokeza kwa wingi kwenye kliniki hiyo; matibabu na dawa vitatolewa bure kwa kila mwananchi atakayebainika na kugundulika kuwa na magonjwa ya aina yoyote.



"Ndugu zangu asiwaambie mtu, kwenye suala la afya kuna watu wameuza nyumba zao, kuna watu wameuza viwanja, kuna watu wamefilisika biashara zao katika kupambana kuuguza ndugu zao na kuna nyakati ndugu zetu wameshindwa hata kukomboa miili ya ndugu zao kutokana na madeni ya gharama za matibabu.

"Neema hii ambayo Mungu ametupa tukaitumie na mikono ya watumishi wa Mungu ikafungue baraka ili tukapate afya kupitia madaktari wetu hawa," alisema.

Makonda alizitaja hospitali na taasisi zitakazoshiriki kliniki hiyo na kutoa madaktari wake bingwa ni pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali ya Kanda KCMC, Hospitali ya Kanda Benjamin Mkapa, Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Mawenzi, SAIFEE na hospitali na taasisi zingine za ndani na nje ya Mkoa wa Arusha.

**RENTAL AND SALE OF PLANT AND EQUIPMENTS (SLAUGHTER HOUSE OR ABATTOIR)**

The existing beef and mutton Slaughtering and processing plant has a full set of production lines and cool storage for rent, located in the capital City of Dodoma with an area of 5,000 square meters and convenient transportation, which can be used for the production of all products and storage of beef and mutton. In addition, there is an idle standard warehouse of 10,000 square meters for rent, with a height of 12 meters.

Processing plant equipment: Generator sets, refrigeration equipment, cold storage, dried meat production lines ovens, fryers, spin dryers, automatic vacuum packaging machines, gas storage tanks, hot water tanks, tumbling machines, beef jerky slices, hair removal machines, packaging machines and other equipment for rent and sale.

Interested parties can contact us in the following ways.

**Contact numbers (Whatsapp) :-**
**0714424623/0715315881/0745115678**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZEPHANIA LIFA MASANJA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya T 463 AGW. kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/SHI/KAH/1931/2024**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA HATI YA HATIMILIKI YA KIMILA YA KIWANJA

**SIMON MAGITTA NCHAGWA** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya **hati ya hatimiliki ya kimila** ya kiwanja kilichopo **Nyaswega** katika kijiji cha **Magoto** kata ya **Nyakonga** Wilaya **Tarime**.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu naye.

**TAARIFA YA POLISI:**
**PHQ/DAR/KIN/122166/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LAZARO WASHINGTON KIRUMI anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya HONDA-XL yenye usajili namba: T 615 AFP, CHASSIS NAMBA: MD221006680. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/SHI/KAH/4592/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 14024/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE TIMOTHEO ADAM MWAKATAGE**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by GAINA ELIA KASALILA..............................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

ALL PERSONS claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 8th day of July, 2024.
Dated at Kyela this 13th day of June, 2024.

..................................
*SENIOR RESIDENT MAGISTRATE*

## KUPOTEA KWA CHETI



**DENISI CORNEL KABAKAMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE **(FORM 4)** CHENYE NAMBA ZA USAJILI **S2761-0120**, KILICHOTOLEWA NA SHULE YA SEKONDARI YA **KEREZANGE** MKOA WA **DAR ES SALAAM** MWAKA **2015.** KWA YOYOTE ATAKAEKIONA ATOE TAAFIFA KITUO CHA POLISI.
**TAARIFA YA POLISI:PHQ/RUK/NKA/2698/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19698 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late of tha late JOHN SAMWELI MSASU Of Chilwana Dodoma**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MESHACK SAMWELI MSASU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 24TH Day of JULY, 2024
Dated at Dodoma this 21st Day of JUNE, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MABULA PATER NTOGWA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T456 BRQ, CHASSIS NAMBA: GX1006170287 na ENGINE NAMBA: IGFE1988CC. Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**POLISI TAARIFA :**
**9910841471763**

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT KINYEREZI**
**CIVIL CASE NO. 3073/2024**
**MABRUKI SAMLI t/a NAMELA GENERAL..........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**TUKEKYA SUPPLIES CO. LTD.... DEFENDANT**

**TO: TUKEKYA SUPPLIES CO. LTD**
**P.O.BOX D'SALAAM**
Take notice that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in a plaint filed in this court
Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are defected to collect copies of the summons and plaint from the court's registry.
You are hereby summoned to appear in this court in person or by an advocate or an agent duly authorized on 24-06-2024 at 8:30 am when this suit will be mentioned.
Take further notice that should you default to enter appearance in court on the day time mentioned above, the suit will proceed and judgment may be given in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this day of 20-06-2024

..................................
RESIDENT MAGISTRATE

## NGOMENI ENTERPRISES

### INIVITATION FOR TENDER CLOSED BIDS

We, **NGOMENI ENTERPRISES LIMITED** working on behalf of **CRDB BANK PLC** invites general public and interested buyers to submit closed bids for purchasing commercial cum residential landed properties belonging to **Emmanuel Elisante & Frank Rwekiza Machume** with details stated hereunder.

**DETAILS OF THE PROPERTY TO BE SOLD**

| SN | DESCRIPTION | REGISTRATION DETAILS | PHYSICAL LOCATION | DEADLINE OF SUBMISSION (DAY, DATE AND TIME |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Landed properties | Certificate of Title Number 82837, Land office No. 350952. | Located on Plot Number 109, Block "47", Kijitonyama area in Dar es salaam. | Friday , 12nd July, 2024, before 10:30 Hours |
| 2. | Landed properties | Certificate of Security arrangement | Residential property located at Bomba area in Kongowe. | Friday, 12nd July, 2024, before 10:30 Hours |

**CONDITIONS AND REQUIREMENTS OF BID SUBMISSION**

1. The sale will be conducted through OPEN COMPETITIVE TENDERING PROCESS. The bids MUST be addressed and submitted during WORKING DAYS AND HOURS to NGOMENI ENTERPRISES LIMITED Office located at NEADA PLAZA, 2ND Floor,Kimara Temboni, Saranga Road, Ubungo District, Dar es Salaam City, Tanzania.
2. Bids should be submitted in sealed envelopes clearly marked "PURCHASE **OF A LANDED PROPERTY** and all closed bids shall be opened on Friday, 12nd July, 2024, before 10:30 Hours at Our Office.
3. Upon receiving notification of award, the winner/buyer will be required to deposit 25% of the bid price within 24hours, whereas the remaining 75% will be paid within 14 days from the date of receipt of notification of award. Failure to pay the remaining 75% will result into forfeiture of the already deposited funds and the BID process will be repeated. All Payments should be made through CRDB Bank PLC account to be provided by NGOMENI ENTERPRISES and the Transfer shall clearly indicate name of the Bidder.
4. Any bidder will be required to fill in a prescribed form which shall be submitted as a bid declaration form, obtained at Our Office.
5. Interested bidders may inspect a property immediately after the publication of this advertising starting from 10:00 AM to 2:00 PM at own expenses including transport after consultation with Our Office.
6. Transfer of ownership charges and payment of relevant levies and taxes shall be borne by the successfully bidder.
7. The property shall be sold on the 'as is where is basis'
8. Bids submitted after the set deadlines will NOT be received.

**CONTACT US FOR MORE DETAILS AND INQUIRIES THROUGH,**

MANANGING DIRECTOR,
NGOMENI ENTERPRISES,
NEADA PLAZA BUILDING,
2ND FLOOR, KIMARA TEMBONI,
SARANGA ROAD, ROAD, P O BOX
36359
**DAR ES SALAAM**

MOB:0753575752
Email: ngomenienterprises@gmail.com

## SUKAH SECURITY AUCTION MART CO.LTD
## (WATU WA KAZI)

HEAD OFFICE:
P.O.Box 10751 DVN Bldg.
Postal Road – Mwanza
Mob: 0754 860 435, 0715- 860 435

Dealers in:
Day and Night Safe Guards,
Security Consultants,
Rapid Ambulance response,
Dog Unit and Mobile Patrolling,
Debt Collector and General Auctioneers

KAGERA BRANCH:
P.O.Box 574
Mob0755 003370
KARAGWE

## NOTICE / TAGANZO

Sukah Security Company (T) Limited Auction Mart kwa idhini tuliyopewa na Mteja wetu **NCBA BANK TANZANIA LTD** tunatoa notisi ya siku thelathini (30) na tangazo la mnada kwa wadaiwa kulipa deni unalodaiwa vinginevyo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara na Zabuni ya dhamana za mikopo hiyo.

| Na. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALA ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1. | Osward Ackim Mwandumsya | Nyunba Plot. No. 251- 253 Block "A" TITLE: Deed No. 30102 L.O. No. 417660 | KISEKE Mwanza Mjini Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 4:00 asubuhi na kuendelea |
| 2. | Emmanuel Mwikabe | Nyumba Plot. No. 68 Block J CT No. 31705 | Buswelu – Ilemela Mwanza Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 5:00 asubuhi na kuendelea |
| 3. | Raphael Mwita Meti | Nyumba No.265 Block CT No.31463 | Nyakato Nyamagana Mwanza Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 6:00 asubuhi na kuendelea |
| 4. | Deogratis Enosy Mirobo | Nyumba plot. No.62 Block "B" Title Deed No. 21499 | Nyegezi Nyamagana Mwanza Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 7:00 asubuhi na kuendelea |
| 5. | Plot No. 330 Block 'L' | Title Deed No. 68645 | Nyakato Mwanza Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 8:00 mchana |
| 6. | Plot No. 810 Block 'D' | Title Deed No. 763 | Isamilo Mwanza Tarehe ya mnada 14/7/2024 Muda: 9:00 mchana |
| 6 | Plot No. 314 Block 'U' | Title Deed No. 13235 | Kambarage Shinyanga Tarehe ya mnada 16/7/2024 Muda: 4:00 asubuhi na kuendelea |
| 7. | Plot No. 8 Block 'R' | Title Deed No. 5395 | Shinyanga Township Tarehe ya mnada 16/7/2024 Muda: 5:00 asubuhi na kuendelea |
| | Geofrey Maliyawonda | Nyumba plot.no.616 Block "S" TITLE DEED No. 36359 office no 3891184 | Mbulu kahama Tarehe ya mnada 16/7/2024 Muda: 8:00 mchana |

**KWA MAWASILIANO YA ZABUNI**
**SIMU NA. 0754 860435**

## Mvutano kuwania nafasi kiongozi upinzani waendelea DRC

**KINSHASA,** DRC

VITA vya kuwania nafasi ya kiongozi wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), bado inaendelea jambo linalosababisha upinzani katika taifa hilo kushindwa kuungana hadi sasa.

Inaelezwa kuwa nafasi hiyo ilipangwa tangu 2007 lakini haijawahi kushikiliwa kwa sababu ya tofauti za siasa za upinzani.

Kambi ya mwanasiasa wa upinzani Moïse Katumbi iliyozindua upya utaratibu huo mwezi huu, lakini ikacheleweshwa na Martin Fayulu ambaye muungano wake ulikuwa umesusia uchaguzi wa wabunge. Huku wapinzani wengine wakitoa msimamo wao kuhusu suala hilo.

Ilielezwa kuwa msemaji huyo anateuliwa na wabunge na maseneta wa upinzani ndani ya Bunge la DRC. Na kwamba moja ya vigezo atatakiwa kuwa na cheo cha waziri wa nchi na atasimamia bajeti ya kila mwaka.

Katika mtazamo wake, Moïse Katumbi amepata uungwaji mkono wa mawaziri wakuu wa zamani Matata Mponyo na Adolphe Muzito, waliowakilishwa katika Bunge la taifa. Ikielezwa kuwa wapinzani hao wawili wana wabunge wanne pekee huku Moïse Katumbi akiwa na zaidi ya ishirini.

Kwa upande wa mrengo wa Martin Fayulu, hakuna suala la kuteua msemaji baada ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa Desemba 2023, msimamo ambao pia unaungwa mkono na Chama cha Delly Sesanga, kilichoshirikiana na Moïse Katumbi katika uchaguzi wa urais.

Hata hivyo, Chama cha Envol kinaamini kwamba kutokana na hali ya sasa ya kuvunjwa kwa taasisi na kudhoofika kwa demokrasia kimaadili na kisiasa, hadhi ya kitaasisi ya upinzani inasalia kuwa njia isiyofaa kusikika sauti ya watu wanyonge.

Vile vile, chama hicho kinaeleza kwamba mkakati huo hauwezi kutetea watu walioelekezwa kwenye taabu za kijamii, walionyimwa haki zao, uhuru na kuwekwa katika ukosefu wa usalama.

Pia wapinzani wengine walipendekeza marekebisho ya sheria ili kuruhusu vyama visivyo na wawakilishi wa kuchaguliwa katika bunge kushiriki katika zoezi la kupiga kura. **RFI**

# Wawili wajitosa kuchuana na Kagame uchaguzi Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

BAADA ya kufunguliwa rasmi kwa kampeni za uchaguzi mkuu nchini Rwanda wanasiasa wawili kutoka vyama pinzani wamejitosa kuchuana na Rais wa taifa hilo, Paul Kagame katika kinyang'anyiro cha kuwania kiti cha urais.

Wapinzani hao ni Frank Habineza kutoka Chama cha Democratic Green na mwandishi wa habari wa zamani Philippe Mpayimana, anayeshiriki kama mgombea binafsi, baada ya wanasiasa wengine kuzuiliwa kushiriki katika kinyang'anyiro hicho.

Mahakama za Rwanda zilikata rufani za wanasiasa vigogo wa upinzani Bernard Ntaganda na Victoire Ingabire za kuwafutia hatia walizokutwa nazo miaka ya karibuni ambazo kwa sheria za nchi hiyo zinawazuia kuwania kiti cha urais.

Tume ya Uchaguzi pia ilimpiga marufuku mkosoaji mkubwa wa Kagame, Diane Rwigara ikisema ameshindwa kutoa nyaraka zinazoonesha rekodi yake ya uhalifu kama inavyotakiwa kisheria na kwamba hakutimiza takwa la kukusanya saini 600 za raia wanaomuunga mkono.

**Hakuna kitu bora zaidi ya kuwa Mnyarwanda, lakini ni muhimu zaidi, ni mimi kuwa kiongozi wenu... nimekuja hapa kuwashukuru, siyo kuomba kura zenu.**

Diane, mtoto wa tajiri Assinapol Rwigara aliyekuwa mfadhili mkubwa wa Chama cha Kagame cha RPF hadi walipotumbukia kwenye msuguano, alikamatwa na kuzuiwa kugombea urais mwaka 2017 kwa madai ya kughushi nyaraka. Na kwamba baadaye mashtaka hayo dhidi yake yalifutwa.

Katika uchaguzi huo wa Julai 15 Kagame anatarajiwa kurefusha utawala wake wa miaka 24 kwenye taifa hilo.

Wanyarwanda takribani milioni 9 wameandikishwa kushiriki uchaguzi huo wa urais ambao kwa mara ya kwanza utafanyika sambamba na ule wa bunge.

Akizungumza kwenye mkutano wa ufunguzi wa kampeni uliohudhuriwa na maelfu ya wafuasi wake, wengi wakiwa wamefikishwa hapo kwa mabasi, Kagame alitetea rekodi ya nchi yake kwenye suala la demokrasia. Huku matamshi yake yakillenga kuwafunga midomo wale wanaoutuhumu utawala wake kwa kukandamiza upinzani na kutawala na mabavu.

"Kwa kawaida watu hutofautiana kuhusu demokrasia au huielewa dhana hiyo kwa namna tofauti. Lakini kwetu sisi, tunayo tafsiri yetu ya (demokrasia). Demokrasia maana yake ni kuwepo chaguo, kuchagua kati ya kizuri kwako na kile unachokitaka," alisema Kagame.

"Hakuna kitu bora zaidi ya kuwa Mnyarwanda, lakini ni muhimu zaidi, ni mimi kuwa kiongozi wenu... nimekuja hapa kuwashukuru, siyo kuomba kura zenu," alisema Kagame.

Rais Kagame aliingia madarakani rasmi kuwa rais mwaka 2000 kwa kuchaguliwa na bunge baada ya kujiuzulu kwa Rais Pasteur Bizimungu.

Tangu wakati huo ameshinda chaguzi tatu kwa zaidi ya asilimia 90 mwaka 2023, 2010 na 2017. Huku katika uchaguzi wa mwisho wa 2017, akijizolea asilimia 99 ya kura.

Kiongozi huyo amekuwa akipata sifa kwenye jukwaa la kimataifa kwa kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini Rwanda baada ya mauaji ya kimbari lakini anaandamwa na ukosoaji wa kila wakati kuhusu rekodi dhaifu ya haki za binadamu na ukandamizaji wa kisiasa.**DW**





Wagombea urais Rwanda, Rais Paul Kagame (kushoto), Frank Habineza na Philippe Mpayimana. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Mauritania ashauri Afrika Magharibi kuungana

**NOUAKCHOTT,** Mauritania

RAIS wa Mauritania, Mohamed Ghazouani, ametoa wito kwa nchi za Afrika Magharibi kuungana pamoja katika kukabiliana na jihadi, kabla ya uchaguzi wa rais unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni nchini humo.

Ghazouani aliliambia shirika la habari la AFP jana kwamba eneo hilo lazima litengeneze utashi wa pamoja wa kisiasa ili kupambana na ukosefu wa usalama.

"Mimi sio mmoja wa wale wanaofikiri leo kwamba nchi zinaweza kukabiliwa na tishio kama ugaidi," alisema.

Mkuu huyo wa zamani wa jeshi na waziri wa ulinzi mwenye umri wa miaka 67 anatazamiwa kuwania muhula wa pili kama kiongozi wa taifa hilo lenye watu milioni 4.5 ambalo liko kimkakati kati ya kaskazini na kusini mwa jangwa la Sahara.

Aliliambia shirika la AFP kwamba hali ya usalama katika eneo hilo dogo sio nzuri kabisa na imekuwa mbaya. **VOA**

# WASHIRIKI WA MBIO ZA DODOMA MARATHON KUTUMIA TRENI SGR

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa mbio za Dodoma Marathon wameingia makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji na Shirika la Reli Tanzania (TRC), yanayotoa fursa kwa washiriki wa mbio wakazi wa jijini Dar es Salaam kutumia Treni ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR), kwenda kushiriki mbio hizo jijini Dodoma na kurudi.

**Kupitia makubaliano hayo inatarajiwa kuwa washiriki zaidi ya 1,000 wa mbio hizo kutoka jijini Dar es Salaam watatumia usafiri huo wa haraka na wa kisasa zaidi ili kushiriki mbio hizo zitakazofanyika Julai 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.**

Lengo kuu la mbio hizo ni kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Hafla ya kusaini makubaliano hayo imefanyika mwishoni mwa wiki kwenye Ofisi za TRC jijini Dar es Salaam ikihusisha viongozi waandamizi na maofisa wa pande zote mbili ambapo ilishuhudiwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa na Mkurugenzi wa Fedha wa waandaaji wa mbio hizo, Waziri Barnabas, wakisaini makubaliano hayo kwa niaba ya taasisi zao.

Hafla hiyo ilitanguliwa na safari ya wadau hao kutoka jijini Dar es Salaam hadi Morogoro na kurudi hatua ambayo hutoa fursa kwa maofisa wa waandaaji hao na wadau wengine wakiwamo baadhi ya wakimbiaji kutoka klabu mbalimbali za wakimbiaji jijini Dar es Salaam kuweza kupata uzoefu wa usafiri huo kabla ya safari hiyo inayotarajiwa kufanyika siku moja kabla marathon hiyo.

"Ushirikiano huu ni pamoja na kutoa fursa kwa washiriki wa mbio zetu kutoka jijini Dar es Salaam na Morogoro kwenda jijini Dodoma, pia unalenga kuthibitisha dhamira yetu kama taasisi katika kuunga mkono jitihada kubwa zilizofanywa na serikali hadi kufanikisha mradi huu mkubwa na wa kisasa.

"Ili kujijengea uzoefu na kuwa mashuhuda kwa washiriki wa mbio zetu watakaotumia usafiri huu siku chache zijazo, sisi kama benki na wadau wetu wengine wakiwamo wadhamini tumetumia usafiri huu leo ili kujionea ubora wake ambao kiukweli umetuvutia sana...pongezi kubwa kwa serikali na TRC kwa hatua hii muhimu," alisema Waziri.

Kwa mujibu wa Waziri matumizi ya treni hiyo yatatoa fursa ya chaguzi zaidi za aina ya usafiri kwa washiriki wa mbio hizo kutoka jijini Dar es Salaam kwa kuwa wapo washiriki wengine ambao watatumia aina nyingine za usafiri ikiwamo mabasi, magari binafsi na ndege.

"Pamoja na aina nyingine za usafiri, washiriki watakaopata fursa ya kutumia treni hii ya SGR watahakikishiwa burudani mbalimbali mwanzo hadi mwisho wa safari wakiwa kwenye mabewa yatakayoandaliwa mahususi kwa ajili yao," aliongeza.

Awali akizungumza kwenye tukio hilo, Kadogosa alisema ushiriki wa shirika hilo kwenye mbio hizo unalenga kuunga mkono agenda ya kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake na kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wanaosomea taaluma ya ukunga ili kuboresha afya ya mama wa mtoto.

Aidha, aliwahakikishia washiriki wa mbio hizo kupata huduma na uzoefu wa kipekee hasa kutokana na ukweli kwamba safari hiyo itakuwa ni miongoni mwa safari za mwanzo za treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.



Wadau wa mbio za Dodoma Marathon wakifanya safari kwa kutumia treni ya mwendokasi (SGR), kutoka jijini Dar es Salaam hadi Morogoro na kurudi, lengo likiwa ni kupata uzoefu wa usafiri huo kabla ya safari yao ya kuelekea Dodoma inayotarajiwa kufanyika siku moja kabla ya mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Julai 28, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kocha KMKM na sababu JKU SC kuipoka ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM SC imemaliza msimu wa Ligi Kuu Zanzibar 2023/2024 kwa kushindwa kutetea taji lake baada ya kuambulia nafasi ya tatu kwa kujikusanyia alama 57 katika michezo 30 iliyocheza.

KMKM kwa msimu huu mbio za ubingwa zilikuwa ngumu kwao baada ya JKU SC na Zimamoto kukimbizana hadi mchezo wa 30, ambao uliipa ubingwa JKU.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa KMKM, Ame Msimu, alisema si kama ulikuwa msimu mbaya bali ushindani mkali wa Ligi Kuu kwa msimu huu ndio umesababisha kutofurukuta katika mbio hizo katika hatua za mwishoni.

Alisema klabu zote za Ligi Kuu Zanzibar katika mzunguko wa awali zilionesha upinzani mkubwa kuhakikisha kila moja inamaliza mzunguko huo ikiwa kwenye nafasi nzuri na hata mzunguko wa lala salama uliendelea hivyo.

Alisema uwapo wa udhamini katika ligi hiyo, ndio uliosababisha klabu za Ligi Kuu kujinoa vema na kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa na wanaoweza kupambana.

"Msimu huu ligi ilikuwa ngumu sana uwanjani, kila timu iliijiandaa vema kwa kufanya usajili mzuri ambao utaipa matokeo mazuri,"alisema.

Aidha, alisema ugumu huo wa ligi na ushindani mkubwa ndio uliosababisha kutojulikana kwa bingwa mapema, lakini pia hata timu zinazoshuka daraja kushindwa kujulikana mapema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wataanza maandalizi mapema kuhakikisha wanapata muda mkubwa wenye utulivu ili kuhakikisha msimu mpya wa ligi wanaanza kwa kutoa ushindani mkubwa.

KMKM katika michezo 30 iliyocheza imeshinda 18, sare mitatu na kufungwa mechi tisa.

# *Goran Kopunovic aenda Zenji kusaka wachezaji*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Pamba, Goran Kopunovic, amekwenda mjini Zanzibar kusaka baadhi ya wachezaji ambao atawasajili kwenye kikosi chake kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Moses William, amesema kocha Goran alidokezwa kuwapo kwa baadhi ya wachezaji wazuri ambao wanaweza kuipa mafanikio timu hiyo iliyopanda Ligi Kuu, hivyo kwenda visiwani humo kwa ajili ya kuwaangalia.

"Kocha wetu yupo Zanzibar, Ligi Kuu visiwani inaendelea, alipewa taarifa kuwapo kwa wachezaji wazuri ambao kama akiwasajili kwenye timu wanaweza kuipa mafanikio, kwa hivi ninavyozungumza ni kweli yupo huko, na mambo yakienda vizuri hivi karibuni tutawatangazia ni wachezaji gani ambao tumewasajili," alisema Ofisa Habari huyo.

Kocha huyo wa zamani wa Simba, msimu huu akiwa amefundisha Tabora United, alitangazwa wiki iliyopita kuchukua mikoba ya Mbwana Makata ambaye ameipandisha daraja timu hiyo.

Ofisa Habari huyo pia alikanusha taarifa kuwa klabu hiyo imeita wachezaji kwa ajili ya majaribio. Alisema hakuna kitu kama hicho na klabu itasajili wachezaji kufuatana na matakwa ya benchi la ufundi na siyo kukusanya wachezaji pamoja na kuwafanyia majaribio.

"Kitu hicho hakuna, ni uzushi tu, kama ninavyokwambia kocha wetu yupo Zanzibar na amewapa kazi watu wengine kuwapata wachezaji ambao anahitaji," alisema Moses.

Pamba, iliyoshuka daraja mwaka 2001, ilipanda msimu huu, ikishika nafasi ya pili nyuma ya KenGold.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### DOMINIC ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle inakaribia kumsajili Dominic Calvert-Lewis mwenye umri wa miaka 27, ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Everton. ***(Guardian)***

#### KILMAN NAYE AWINDWA

NEWCASTLE pia imetoa ofa ya fedha pamoja na mchezaji kwa beki wa kati wa Wolves, Max Kilman mwenye umri wa miaka 27. ***(Telegraph)***

#### ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL imewasilisha ombi la kumnunua beki wa pembeni wa Fenerbahce, Ferdi Kadioglu mwenye umri wa miaka 24. ***(Ajan Spor)***

#### LUIZ HUYOOO JUVENTUS

MCHEZAJI wa Aston Villa, Douglas Luiz, anakaribia kuhamia Juventus na anatazamiwa kufanyiwa vipimo vya afya wiki ijayo nchini Marekani, ambapo kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, yuko kwenye majukumu ya Copa America na Brazil. ***(Gianluca)***

#### OLISE MALI YA BAYERN

MANCHESTER City na Manchester United zilichukua hatua za kuchelewa kumsajili Michael Olise, ambaye anatarajiwa kujiunga na Bayern Munich, huku zote zikiangalia uwezekano wa kumruhusu winga huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, kusalia na Crystal Palace kwa mkopo kabla ya kujiunga nao msimu ujao. ***(Mirror)***

#### SOULE AULIZIWA

ASTON Villa imeuliza kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Matias Soule mwenye umri wa miaka 21, lakini Juventus inasema hauzwi. ***(Sky Sports)***

#### ANSELMINO NA CHELSEA

CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na Boca Juniors kuhusu dili la kumnunua beki wa Argentina mwenye umri wa miaka 19, Aaron Anselmino. ***(Athletic)***

#### ZIRKZEE ANYATIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inajiandaa kutumia kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 33.8 katika mkataba wa mshambuliaji wa Bologna Mholanzi Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23. ***(Telegraph)***

#### SIMONS ALENGWA PSG

KIUNGO wa kati wa Paris St-Germain na Uholanzi, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21, ndiye anayelengwa na Bayern Munich. ***(Bild )***

#### PIOLI ATAJWA AL-ITTIHAD

KOCHA wa zamani wa AC Milan, Stefano Pioli ni miongoni mwa wanaowania kuwa kocha wa Al-Ittihad . ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ASIMAMISHA MECHI EURO MARA NNE

**Mashabiki wanatambua nyota wakubwa, lakini kuna hali ngumu sana ikiwa nia zao si...**

**DORTMUND,** Ujerumani

MCHEZO wa ushindi wa Ureno wa Kundi F kwenye Euro 2024 dhidi ya Uturuki mjini Dortmund Jumamosi, ulisimamishwa mara nne na mashabikii walioingia uwanjani kupiga picha za 'selfie' na Cristiano Ronaldo.

**Kocha wa Ureno, Roberto Martinez, alizungumza kwa maneno mazito kuhusu matukio hayo baada ya mchezo huo akisema hayafai kuruhusiwa kutokea na kuwataka mashabiki wengine kutoiga mfano huo.**

"Ni wasiwasi, lakini leo (juzi) tulikuwa na bahati kwani nia ya mashabiki ilikuwa nzuri," alisema.

"Mashabiki wanatambua nyota wakubwa, lakini kuna hali ngumu sana ikiwa nia zao sio sawa na wachezaji watafichuliwa.

"Haipaswi kutokea. Kuna usalama mwingi, kwa hivyo haipaswi kutokea. Labda kuna ujumbe kwa mashabiki kwamba hii si njia sahihi. Ujumbe ni kwamba inaweza kuwa mbaya zaidi kwa siku za usoni na si vizuri wachezaji wanawekwa wazi sana uwanjani."

Ronaldo, ambaye sasa anacheza soka klabu nchini Saudi Arabia akiwa na Al Nassr, alitabasamu na kupiga picha na mvulana mdogo ambaye alikwepa usalama na kukimbilia uwanjani katika dakika ya 70.

Mtoto huyo mwenye umri wa karibu miaka 10, alikumbatiwa na Ronaldo kabla ya kuwakimbia wasimamizi wa usalama hadi akashindwa kutoroka nje ya uwanja.

Alipokuwa akitolewa, wasimamizi na watu wengine waliokuwa kwenye mstari walimpiga kichwani kijana huyo, na umati wa watu waliokuwa ndani ya uwanja ulishangilia huku akipunga mkono na kutolewa nje.

Kijana mmoja kisha akajaribu kurudia mchezo huo dakika 15 baadaye, lakini nahodha wa Ureno Ronaldo alirusha mikono yake hewani na kumpungia mbali kabla ya usalama kumzuia kijana huyo kumfikia mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid na Manchester United.

Mara zote mbili, mwamuzi wa Ujerumani Felix Zwayer alilazimika kuchelewesha mchezo hadi vijana hao walipoondolewa uwanjani.

Wafuasi wengine wawili, wanaume wazima, walikimbia uwanjani katika muda wa kusimama na kuelekea kwa Ronaldo wakiwa na simu zao kabla ya kuzuiwa na usalama.



# NACHO YUPO TAYARI KUELEKEA SAUDIA

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Real Madrid, Nacho Fernandez, anakaribia kusajiliwa na Al Qadsiah inayoshiriki Ligi ya Saudi Arabia, chanzo kimeithibitishia ESPN.

ESPN iliripoti mapema mwezi huu kwamba beki Nacho - ambaye yuko kwenye majukumu ya kimataifa na Hispania katika michuano ya Euro 2024 - alikuwa kwenye mazungumzo na timu nyingine ya Saudi, Al Ittihad.

Hata hivyo, beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 34, alipewa ofa na Al Qadsiah na akitaka kusuluhishwa kwa mustakabali wake haraka iwezekanavyo, hivyo ameamua kukubali, chanzo kilisema.

Nacho ameshinda rekodi ya pamoja ya mataji 26 akiwa na Madrid, baada ya kujiunga na klabu hiyo akiwa na umri wa miaka 11 na kupitia akademi hiyo.

Mkataba wake huko Madrid unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu na alikuwa ametumia wiki za hivi karibuni kufikiria mustakabali wake.

Nacho alikuwa nahodha wa Madrid katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga msimu huu, baada ya kukaribia kuondoka katika klabu hiyo msimu wa majira ya joto wa 2023 kabla ya kuamua kusalia.

Al Qadsiah ilishinda kupanda Ligi Kuu Saudia msimu uliopita na inanolewa na mchezaji wa zamani wa Real Madrid, Michel Gonzalez.

# Roque kutimkia Fiorentina

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Vitor Roque, huenda akahama msimu huu wa majira ya joto, huku ripoti nchini Italia zikidai kuwa Fiorentina wako kwenye mazungumzo ya kumtaka.

Tangu alipowasili kutoka Athletico Paranaense Januari, Roque alikumbana na vikwazo vikubwa katika kujiimarisha kikosi cha kwanza kilichojaa nyota wa Barcelona katika nusu ya mwisho ya msimu wa 2023/24 chini ya Kocha Xavi.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 19, anaonekana kutamani kubakia Barca, huku kocha mpya, Hansi Flick akishika usukani kwa sasa.

Lakini kuhama kunaweza kuamsha ujasiri wake na kutoa uzoefu muhimu na fursa za maendeleo kwa kufikia uwezo wake kamili.

Kulingana na mwanahabari Gianluca Di Marzio, Fiorentina wamewasiliana na wawakilishi wa Roque na Barca ili kuchunguza uwezekano wa kumsajili.

Ripoti hiyo inapendekeza kwamba Fiorentina wako sokoni kutafuta mshambuliaji mpya kwa mkataba wa kudumu na wanataka kuelewa 'uwezekano' wa dili hilo - Roque ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa euro milioni 500.





# *Juventus yamtaka Luiz*

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus inakaribia kukamilisha dili la kiungo wa Aston Villa, Douglas Luiz, chanzo kimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil anatazamiwa kuhamia Turin kwa ada ya takriban pauni milioni 43.

Wachezaji wawili wa Juventus Samuel Iling-Junior na Enzo Barrenechea wanakaribia kuhamia Aston Villa kwa mkataba tofauti wenye thamani ya pauni milioni 18.6.

Chanzo kimeiambia ESPN kwamba mikataba hiyo inaendelea na inapaswa kukamilishwa rasmi mwishoni mwa wiki ijayo.

Kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie awali alikuwa sehemu ya majadiliano kati ya Juventus na Aston Villa, lakini hajajumuishwa katika uhamisho huo.

Luiz, ambaye alihamia Villa Park kutoka Manchester City mnamo 2019, alikuwa sehemu muhimu ya timu ya Kocha Unai Emery msimu uliopita ilipomaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu England na kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Villa imekuwa chini ya shinikizo la kutafuta fedha baada ya kuripoti hasara ya karibu pauni milioni 120 Machi mwaka huu.

Luiz anaondoka Villa akiwa amecheza mechi 204 ndani ya miaka mitano, akifunga mabao 22. Villa pia wamekubali mikataba ya Tim Iroegbunam kujiunga na Everton na Omari Kellyman kujiunga na Chelsea.

## Simba kukwepa ya Uturuki kambi Misri

INATOKA UKURASA 24

kutoka nchini Nigeria zinasema mchezaji huyo amekubali kujiunga na kikosi hicho, ambapo amepata ofa ya mkataba wa miaka mitatu.

"Kila kitu kimekwenda vizuri na kilichobaki ni kutia saini tu, mazungumzo baina ya pande zote mbili yamekamilika," kilisema chanzo hicho.

Mchezaji huyo aling'ara msimu uliomalizika kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na kuwavutia mabosi wa Simba ambao kwa sasa wako kwenye hatua za mwisho kumaliza dili hilo.

Ahmed amewaambia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa usajili wa safari hii utakuwa mkubwa, kwani watasajiliwa wachezaji wenye viwango vya juu, kwa kuwa anayefanya kazi hiyo ni mwenyewe, Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohameed Dewji.

"Ule usajili wa kusuasua umeshapitwa na wakati, anayeongoza mashambulizi safari hii ni Mo mwenyewe," alisema.

## Yanga yashtukia mawakala wa wachezaji

INATOKA UKURASA 24

taarifa zilizokuja baadaye zikaeleza, Simba imepindua meza na kumsainisha mkataba wa miaka mwili.

Hata hivyo, bado Simba haijathibitisha rasmi kumsajili mchezaji huyo mpaka sasa.

Akizungumzia usajili, Kamwe alisema tayari wameshamaliza kazi iliyobaki ni kuwatangaza tu.

Tangu awali, Yanga ilitangaza kuwa haitofanya usajili mkubwa sana kwani bado ina kikosi imara, na ilichofanya ni kuzuia wachezaji wake muhimu kubaki, na kufanya usajili wa wachezaji wachache tu wenye viwango vya hali ya juu kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi.

"Malengo tuliyonayo ni makubwa na usajili tulioufanya, watu watalia na kusaga meno," alisema Kamwe.

Tetesi zinadai kuwa Yanga imekamilisha usajili wa wachezaji, Emmanuel Bola Lobota, winga kutoka Singida Black Stars, Agee Basiala, kiungo mshambuliaji kutoka AS Maniema Union na beki wa kushoto, Chadrack Boka kutoka Klabu ya Saint Eloi Lupopo, wote hao kutoka DR Congo.

Mwingine ni kipa Khomein Abubakar wa Singida Black Stars, anayekwenda kuchukua nafasi ya Metacha Mnata, anayetajwa kuondoka msimu ujao.

# SERIKALI KUJA NA MPANGO WA NCHI NZIMA KUFANYA MAZOEZI

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, wanaandaa mpango wa nchi nzima wa kushiriki michezo mbalimbali ya kushughulisha mwili ikiwamo mpira wa miguu na yoga ili kukabiliana na magonjwa yakiwamo yasiyoambukiza, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Yoga, iliyoandaliwa na Ubalozi wa India nchini.

Maadhimisho hayo kwa mwaka huu yamebebwa na kaulimbiu isemayo "Yoga kwa ajili ya mtu binafsi na kwa ajili ya jamii nzima."

**Msigwa alisema kwa sasa wizara hizo zipo kwenye mazungumzo kuhusu suala hilo ambapo mpango huo ukikamilika utahusisha pia, mazoezi ya kukimbia na michezo mingine.**

"Siku ya Yoga ni muhimu kwa kuwa maudhui yake yanafaida kwa mtu binafsi na kwa jamii kama kaulimbiu isemavyo 'Yoga ni sehemu ya kujenga mwili. Kila mmoja akiamua mazoezi kuwa sehemu ya maisha yake atakuwa na afya njema na kukabiliana na magonjwa," alisema.

Alisema wataalamu wanasema sehemu kubwa ya maradhi yanayosababisha vifo vya watu duniani kwa sasa ni yale yasiyohusisha kuushughulisha mwili.

Alisisitiza kuwa mtu akiwa na afya mbovu atatumia fedha nyingi katika matibabu, lakini mwenye afya njema atafanya kazi na kujenga uchumi binafsi na wa taifa.

Mwakilishi wa Balozi wa India nchini, Naibu Balozi Manoj Verma, alishukuru wadau mbalimbali waliojitokeza katika maadhimisho hayo yaliyohusisha pia wanafunzi kutoka shule mbalimbali.

Alisema mazoezi ya yoga yanahusisha upumuaji, kulegeza viungo vya shingo, mikono na miguu, jinsi mtu anavyotakiwa kusimama na kukaa na mikao ya kuegemea na kutafakari kwa kina.

Neema John ambaye ni mmoja wa washiriki wa mazoezi hayo, alisema mazoezi hayo ni mazuri na muhimu kwa wale ambao hawawezi kushiriki michezo kama kukimbia au kutembea mwendo mrefu, kwa kuwa hayatumii nguvu bali viungo vya mwili na akili.

Yoga inatambuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), na mazoezi yake huhusisha vitu viwili, viungo vya mwili na fikra ambapo mtu anapata muda wa kufanya tafakuri kwa kukaa kimya peke yake hivyo kuimarisha afya ya akili.

## KWISHA KAZI...



Kiungo wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Romania katika mechi ya michuano ya Euro 2024, nchini Ujerumani juzi. **PICHA: MTANDAO**

## *Coastal Union yahamia kwa Abuya wa Singida*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imetajwa kuwa iko mbioni kumsajili kiungo mshambuliaji raia wa Kenya anayeichezea Klabu ya Singida Black Stars, Duke Abuya, ikiwa ni mikakati ya maandalizi ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa kwa sasa ipo kwenye mazungumzo na mchezaji huyo ambaye kwa sasa amemaliza mkataba na klabu yake hiyo.

Hata hivyo, habari zinaeleza klabu yake hiyo ipo kwenye jitihada kubwa za kumshawishi kubaki, lakini mwenyewe anaonekana kutaka kwenda kucheza michuano ya kimataifa kwa lengo la kujiweka sokoni.

"Tuko kwenye mazungumzo naye, hatujamaliza, lakini ameonyesha kukubali na anataka kucheza mechi za kimataifa na sisi tumemwambia aje kwetu, akicheza Kombe la Shirikisho ataonekana, lakini klabu yake nayo inamshawishi abaki, mwisho wa siku tutaona, lakini tuna nafasi kubwa ya kumpata," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya Coastal Union.

Hivi karibuni, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El Sabri, alisema wako kwenye mikakati kabambe kuhakikisha wanasajili wachezaji bora na wazoefu wa mechi za kimataifa, ili kushiriki vema michuano hiyo na haiendi kusindikiza. Mmoja wa wachezaji ambao alikiri kuwa nao kwenye mazungumzo ni beki wa zamani wa AS Vita ya DR Congo na Yanga, Djuma Shaaban.

"Ni kweli tupo kwenye mazungumzo na Djuma, ni mchezaji mzuri, mzoefu katika mechi za kimataifa. Unajua tangu tulipopata nafasi ya kucheza Kombe la Shirikisho, tayari kama klabu tukatambua mahitaji yetu," alisema.

Pamoja na kumtaja mchezaji mmoja tu, lakini habari zinaeleza kuwa klabu hiyo ilikuwa kwenye mazungumzo na wachezaji Saido Ntibazonkiza aliyeachwa na Simba, pamoja na winga wa zamani wa Yanga na RS Berkane ya Morocco, Tuisila Kisinda ambaye amemaliza mkataba wake na klabu hiyo.

# Michezo

Jumatatu Juni 24, 2024

Nipashe



Juventus yamtaka Luiz UKURASA 22

## 'SELFIE' KWANZA...



Mtoto aliyewatoroka walinda usalama katika Uwanja wa Signal Iduna Park, Ujerumani na kuingia uwanjani hapo wakati mpira ukiendelea kwa lengo la kupiga 'selfie' na mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo. Jambo lililosababisha mpira kusimama kwa dakika kadhaa. Katika mechi hiyo ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa usiku wa kuamkia jana, Ureno iliichapa Uturuki mabao 3-0. **HABARI UK, 21. PICHA: MTANDAO**

# Simba kukwepa ya Uturuki kambi Misri

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewatoa hofu wanachama na mashabiki wake kuwa itakwenda nchini Misri kuweka kambi ikiwa kamili na si mafungu kama wanavyodhani.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema safari hii wanakwenda wakiwa kamili, ambapo wachezaji wote walioongezwa mikataba na wapya waliosajiliwa, pamoja na jopo lote la makocha litaondoka pamoja kwenda Ismailia nchini humo kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.**

### ●●● Nyota wote sasa safari moja huku mambo yakinyoka kwa kiungo mkabaji Mnigeria ambaye...

"Timu ikiondoka hapa Tanzania mwanzoni mwa mwezi wa saba, tutaondoka tukiwa kamili, kwa maana ya makocha wote; mkuu, msaidizi, wa makipa, wa viungo na meneja, kila mtu atakuwa kwenye nafasi yake, pia tutaondoka wote pamoja hapa hapa na wachezaji wote walioongezewa mikataba na wapya, kuelekea kambini kuanza 'pre season' yetu," alisema Ahmed.

Alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa na wasiwasi, kwani moja kati ya vitu ambavyo viliifanya Simba kutofanya vyema msimu uliopita ni wachezaji wake kuonekana hawana stamina, na hii ilichangiwa na kikosi kwenda nchini Uturuki kimafungu.

Katika kuanza msimu uliomalizika, kikosi hicho kilikwenda kupiga kambi yake nchini Uturuki, katika namna ya kushangaza ilikwenda na baadhi ya wachezaji wachache, wengine wakibaki nchini kwa sababu mbalimbali za kimikataba, wengine kukosa viza.

Baadhi ya wachezaji walisajiliwa wakati 'pre season' inaendelea, na walipofika zilibaki siku chache tu kabla ya kurejea, hivyo wakashindwa kuwa na utimamu wa mwili.

"Tunatarajia kuweka kambi huko, ambapo tathmini yetu imetuonyesha ya kwamba hali ya hewa ni rafiki kwa timu, hoteli tunayokwenda kufikia ni ya kisasa, hapo hapo kuna gym, ina viwanja visivyopungua vinne," alisema Meneja Habari huyo.

Wakati hayo yakiendelea klabu hiyo imetajwa ipo katika hatua za mwisho kupata saini ya kiungo mkabaji raia wa Nigeria, Augustine Okejepha mwenye umri wa miaka 20, kutoka Klabu ya Rivers United.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo na vyanzo vingine

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga SC yashtukia mawakala wa wachezaji

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imesema kuwa baadhi ya mawakala wanaitumia klabu hiyo kwa ajili ya kuwapa thamani wachezaji wao na kuwauza kwa dau kubwa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema baadhi ya mawakala wa wachezaji wamekuwa na tabia ya kuwahusisha wachezaji kuwa wanatakiwa na Yanga ili kuzifanya timu zingine zipande dau wakati si kweli kama wanawahitaji.

Kamwe alisema vitendo hivyo vilifanyika msimu uliopita na anashangaa msimu huu vimeibuka tena, akiwataka mawakala kuwauza wachezaji kwa thamani zao halisi na kuacha kuitumia Yanga kwa njia ya kuwapandisha thamani na kupata pesa nyingi za usajili.

"Mwaka jana hawa mawakala walitengeneza stori kuwa kuna mchezaji Yanga inamtaka, lakini alipokwenda klabu nyingine ikasemekana eti ameibiwa Uwanja wa Ndege, sisi wala hatukusema kitu," alisema Kamwe.

Ingawa hakufafanua, lakini ukirejea moja ya stori za matukio ya msimu uliopita ilisemekana kuwa Simba ilimpora mchezaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fabrice Ngoma, Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere, akiwa anakuja kusaini mkataba Klabu ya Yanga.

"Kuelekea msimu unaokuja tunaanza kusikia tena habari kama zile, wanasema kuna kiungo tumepokonywa, si kweli ukiona hivyo hatukumhitaji, hivyo ni kazi ya mawakala kupiganisha ili wapige pesa," alisema Ofisa Habari huyo.

Hivi karibuni katika tetesi za usajili inadaiwa ilikuwa katika hatua za mwisho kumsajili kiungo mkabaji wa Singida Black Stars, Yusuph Kagoma, lakini

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >